# RATIBA YA KONGAMANO LA 10 LA KIMATAIFA LA CHAUKIDU

## KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA KATIKA ZAMA ZA AI

## *Fursa na Changamoto*

*Chuo Kikuu cha Kibabii*

*Bungoma, Kenya*

*Disemba 13 – 16, 2025*

# RATIBA NA IKISIRI

## KONGAMANO LA 10 LA KIMATAIFA LA CHAUKIDU

**CHUO CHA KIBABII**

**BUNGOMA, KENYA**

**13 – 16 DISEMBA 2024**

CHAUKIDU

Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani

CHAUKIDU

Global Association for the Promotion of Swahili

© CHAUKIDU, 2025

# WADHAMINI

MATBAA YA
**CHAUKIDU**
PRESS

KIBABII UNIVERSITY
KNOWLEDGE FOR DEVELOPMENT

## WADHAMINI WENGINE

CALLiT AFRICA
Computer-Aided Lasting Learning

Your Closest Partner in Education
in Africa and Abroad

WWW.CALLITAFRICA.COM

MBIU PRESS

*Paza sauti ya Kiswahili*

# Shukurani

**Kamati ya Maandalizi**
Iribe Mwangi, *Chuo Kikuu cha Nairobi (Mwenyekiti na Makamu wa Rais wa CHAUKIDU)*
Filipo Lubua, *Chuo Kikuu cha Pittsburgh (Rais wa CHAUKIDU)*
Mussa Hans, *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mkurugenzi wa CHAUKIDU)*
Sarah Ngesu, *Chuo Kikuu cha Southeastern Kenya (Naibu Mkurugenzi wa CHAUKIDU)*
Gordien Ndayikengurukiye, *Chuo Kikuu cha Ualimu Burundi (Katibu Mwenezi wa CHAUKIDU)*
Leonora Anyango, *Chuo Kikuu cha Pittsburgh (Mhazini)*
Leonard Muaka, *Chuo Kikuu cha Howard*
Elias Magembe, *Chuo Kikuu cha American*
Mosol Kandagor, *Chuo Kikuu cha Moi*
Peter Mwangi, *Chuo Kikuu cha Northwestern*
Asmaha Heddi, *Chuo Kikuu cha Kansas*
Juliet Jagero, *Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga*
Isayya Lupogo, *Chuo Kikuu Mzumbe*
Flora Mulema, *Mkereketwa wa Kiswahili*
Said Omar, *Chuo cha MS TCDC*
Patrick Mose, *Chuo Kikuu cha Ohio*
Fred Simiyu, *Chuo Kikuu cha Kibabii (Mwenyekiti wa kamati ya wenyeji)*

**Kamati ya Wenyeji, Chuo Kikuu cha Kibabii**
Fred Simiyu (Mwenyekiti)
Eric Wamalwa
Gladys Kinara
Mekarios Wakoko
Kelly Inyani
Meshak Nyambane
Deborah Kisongochi

**Bodi ya CHAUKIDU**
Filipo Lubua, *Chuo Kikuu cha Ohio (Rais)*
Iribe Mwangi, *Chuo Kikuu cha Nairobi (Naibu Rais)*
Mussa Hans, *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mkurugenzi)*
Sarah Ngesu, *Chuo Kikuu cha Southeastern Kenya*
Gordien Ndayikengurukiye, *Chuo Kikuu cha Ualimu Burundi (Katibu Mwenezi)*
Leonora Anyango, *Chuo Kikuu cha Pittsburgh (Mhazini)*
Kiarie Wa'Njogu, *Chuo Kikuu cha Yale (Mhariri Mkuu)*
Leonard Muaka, *Chuo Kikuu cha Howard (Rais Mstaafu)*
Mahiri Mwita, *Chuo Kikuu cha Princeton (Mwenyekiti, TKU)*
Shani Omar, *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*
Hadija Jilala, *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*
Mwajuma Selemani, *Mwalimu Tanga, Tanzania*
Mosol Kandagor, *Chuo Kikuu cha Moi*
Aldin Mutembei, *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Kamati ya Ikisiri na Ratiba



**Peter Mwangi**
*Mwenyekiti Kamati Ya Ikisiri & Ratiba*

IMEKUWA FAHARI kubwa kwangu kuongoza kamati ndogo ya maandalizi iliyoshughulikia ikisiri na ratiba. Kamati hii ilikuwa na wanachama wafuatao: Prof. Mosol Kandagor, Mwalimu Asmaha Hedi, Dkt. Juliet Jagero, Dkt. Isayya Lupogo, Dkt. Said Omar, na Dkt. Fred Simiyu. Kwa ushirikiano na wanakamati wote, na hasa Rais, Dkt. Filipo Lubua aliyetoa uhariri wa kupigiwa mfano, tuliweza kuzua mada kuu pamoja na mada ndogo za kongamano, ambazo zilivutia jumla ya ikisiri 121 kutoka kwa WanaCHAUKIDU.

Zoezi la kutathmini ikisiri liliwashirikisha wanakamati wote pamoja na baadhi ya wanachama wa CHAUKIDU. Kwa jumla, asilimia 87 ya ikisiri zilipokelewa zilikubaliwa, huku zilizobaki zikihitaji maboresho ya namna moja au nyingine. Hatimaye, mchakato wa kuandaa programu ya kongamano ulifaidi pakubwa kutokana na weledi na juhudi za Dkt. Filipo Lubua na Dkt. Patrick Mose, WanaCHAUKIDU wenye bidii ya mchwa na tajiriba pevu katika masuala ya kiteknolojia.

Ikisiri zote zimepangwa katika vikao sambamba vitano vinavyoangazia mada mbalimbali za kongamano. Hivyo basi, wakongamanaji watapata nafasi ya kujumuika na wawasilishaji tofauti kutegemea ilhamu zao za kiutafiti na ufundishaji.

Kwa niaba ya Kamati ya Ikisiri na Ratiba, natoa shukurani za dhati kwa wanakamati na wanachama wote waliofanikisha mchakato mzima wa kusaka na kutathmini ikisiri, na hatimaye kuandaa programu hii. Tunawatakia kongamano lenye mafanikio makubwa na matokeo chanya kwa kila mshiriki.

Wenu,

**Peter Mwangi, Ph.D.**
Chuo Kikuu cha Northwestern, Marekani

KISWAHILI

KIENEE

# Ujumbe wa Rais wa CHAUKIDU

**WAPENDWA WANACHAUKIDU** na wadau wote wa Kiswahili na lugha za Kiafrika, hayawi hayawi, sasa yamekuwa! Karibuni sana Bungoma, Kenya, katika Chuo Kikuu cha Kibabii, tulikokielekeza kipute cha maandalizi ya kongamano letu kwa takribani miezi 12 iliyopita. Ni furaha iliyoje kukutana tena Afrika Mashariki! Shukurani za dhati ziende kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Kibabii kwa kutukaribisha katika viunga vya chuo chao kizuri. Kwa niaba ya Bodi ya CHAUKIDU, tunawashukuru sana sana!.

Mzunguko wa makongamano yetu ya kimataifa umefana hasa. Baada ya kutoka Arusha, Tanzania mwaka 2023, tulikubaliana mwaka jana kuelekea mjini Havana, Cuba, na kwa mara ya kwanza tukapeleka kongamano la Kiswahili Kusini mwa Amerika. Halikuwa jambo dogo hata kidogo! Historia italikumbuka hilo. Na hapa nipende kutoa shukurani na pongezo kwa aliyetupatia wazo hilo, Ndugu Balozi Humphrey Polepole. Mchango na ushirikiano aliotuonyesha tutaviweka daima katika kumbukumbu zetu.

Ni kweli! CHAUKIDU kimeendelea kukua kwa kasi na kukomaa kuwa nguzo kubwa inayounganisha Waswahili na wadau wa lugha za Kiafrika kutoka pande zote za dunia. Na mwaka huu, tumefika Magharibi mwa Kenya kwa mara ya kwanza. CHAUKIDU—kama wasemavyo vijana wa kisasa—haina kipengele, labda kipengele uje nacho wewe! Sidhani yeyote miongoni mwetu ana kipengele. Sidhani!

Kongamano hili litatukumbusha kwamba, zama tunazoishi sasa si za kawaida. Ni zama za mageuzi ya kiakili na kiteknolojia ambayo hayajawahi kushuhudiwa. Ndiyo maana tukaleta kongamano lenye mada kuu muafaka kabisa: *"Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Zama za AI: Fursa na Changamoto."* Katika zama hizi ambamo AI imeweza kutikisa mifumo ya mawasiliano, elimu, tafsiri, na hata uchumi, tunalo jukumu la kuangalia upya nafasi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika katika dunia hii 'mpya'.

Hilo ni jambo muhimu kwa sababu, japo ujenzi wa mifumo ya AI unafanyika kwa kutumia lugha, tunaelewa kuwa hilo limefanyika kwa kuzingatia misingi ya lugha za Kimagharibi, hasa Kiingereza. Katika hali kama hii, tunapaswa kujiuliza kwa umakini na kwa kina: Lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika zinapata nafasi gani katika mazingira mapya ya teknolojia ya kimataifa? Je, AI inapotumia na kuchakata lugha za Kiafrika, inazingatia ufasaha, usanifu, misingi ya kiisimu, na utamaduni uliomo ndani ya lugha hizi? Je, tunaelewa hatari ya kuwa tu watumiaji wa teknolojia hizi badala ya kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa mifumo ya AI kwa misingi ya lugha zetu kwa kuwa wabunifu?



**Filipo Gao Lubua**
*Rais wa CHAUKIDU*

Maswali haya yanahitaji majibu ya kitaaluma, yenye ushahidi wa kitafiti, yenye mwelekeo wa kisera, na yanayozingatia mustakabali wa vizazi vijavyo. Ndiyo maana kongamano letu la mwaka huu linachukua uzito wa kipekee.

Karibuni sana tujadiliane, tufunzane, na tuweke mikakati ya pamoja. Tuitangazie dunia kuwa nasi hatujabaki nyuma. Tumo! Tumo safarini humo!

Wenu,

**Filipo Gao Lubua**
Chuo Kikuu cha Pittsburgh, Marekani

# Ujumbe wa Mkurugenzi wa CHAUKIDU



**Mussa Hans**
*Mkurugenzi wa CHAUKIDU*

**NDUGU WASHRIKI** wa Kongamano, kwa mara nyingine ninakukaribisheni sana katika Kongamano la 10 la CHAUKIDU linalofanyika katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Baada ya mkutano wake wa kwanza uliofanyika Chuo Kikuu cha Howard mwaka 2015, CHAUKIDU imekwishaandaa makongamano mengine ya kimataifa yapatayo nane yaliyofanyika sehemu mbalimbali ambazo ni Nairobi (2016), Dar es Salaam (2017), Zanzibar (2018), Kampala – (2019), Kilifi (2021), Washington DC (2022) na Arusha- (2023). Mwaka 2024 CHAUKIDU ilishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuratibu Kongamano la Kimataifa la Kiswahili lililofanyika Havana, Kuba.

Tukirejelea makongamano haya tutabaini kwamba yako yaliyofanyika ndani ya Afrika Mashariki na mengine yamefanyika nje ya Afrika Mashariki. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba makongamano haya yanafanyika katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Afrika Mashariki kwa lengo la kutekeleza dhamira ya kueneza Kiswahili katika kila kona duniani. Kwa kawaida makongamano ya CHAUKIDU huwa ni fursa muhimu kwa wadau wa Kiswahili kutangamana na kubadilishana mawazo. Ni matumaini yetu kwamba washiriki wa kongamano la mwaka huu wa 2025 watapata wasaa wa kufahamiana na kubadilishana mawazo kwa manufaa ya sasa na ya baadaye. Kama ilivyo ada, makongamano yetu hutanguliwa na warsha na mwaka huu warsha pamoja na kongamano vinajikita katika mjadala kuhusu nafasi ya Kiswahili na akiliunde (kuanzia sasa AI).

Tuzingatie kwamba nafasi ya Kiswahili kimataifa inaendelea kuimarika kila uchao. Hivi sasa Kiswahili ni miongoni mwa lugha zilizopewa hadhi ya kuwa na siku yake Duniani.

Maadhimisho ya Kiswahili hufanyika kila tarehe saba Julai kuanzia mwaka 2022. Aidha, hivi sasa Kiswahili kimepewa hadhi ya kuwa lugha rasmi katika mikutano mikubwa kama Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC, Umoja wa Afrika na Mkutano Mkuu wa UNESCO. Ni kwa kutambua hatua hii ambayo lugha ya Kiswahili imepiga na kwa kuzingatia maendeleo ya sayansi na teknolojia ulimwenguni, ndio maana tutaona kuna umuhimu wa kujadili kinagaubaga nafasi ya Kiswahili katika zama za AI.

Kwa kufanya hivi wadau wa Kiswahili watapata fursa ya kuchangamkia fursa zitokanazo na maendeleo ya Kiswahili ulimwenguni hususan zama za AI. Karibuni sana tujadiliane kwa pamoja nafasi na fursa ya Kiswahili ulimwenguni. Ninawasihi pia kila mmoja wetu apange kufanya ziara ya kitalii katika mandhari tulivu ya Kibabii.

**Dkt. Mussa Hans**
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

.

# Ujumbe wa Mwenyekiti wa Kamati-Andalizi



**Iribe Mwangi**
*Mwenyekiti, Kamati ya Maandalizi*

WAKONGAMANAJI wapenzi, nina furaha kuwaona nyote katika ukumbi huu wa Chuo Kikuu cha Kibabii. Nawakaribisheni kwenye kongamano hili la 10 la CHAUKIDU. Chuo Kikuu cha Kibabii, kikiongozwa na mmoja wetu katika ulimwengu wa Kiswahiili, Prof. Odeo Ipara, kilitia nia ya kuwa mwenyeji wetu mnamo 2023 tulipokongamana jijini Arusha. Hata hivyo, kutokana na sababu za kutaka kusambaza Kiswahili, ombi hilo halikutimia mwaka jana baada ya kongamano letu la 9 kwenda jijini Havana, Kuba. Hata hivyo, hayawi hayawi huwa! Sasa tuko humu! Ni mara ya tatu kwa Kongamano la CHAUKIDU kufanyika nchini Kenya. Baada ya kongamano la kwanza kufanyika kule Nairobi, na la pili kule Kilifi, mwaka huu tuko katika eneo hili lililotulia vizuri la Bungoma kwa hisani ya Chuo Kikuu cha Kibabii.

Kutokana na sababu anuai, kwa mara ya kwanza, kamati ya kuandaa kongamano hili iliundwa kwa kuchelewa na ikaanza shughuli ya kutafuta wadhamini. Baada ya miezi kadhaa, ilibainika kwamba hilo lilikuwa si rahisi kwa kuwa wengi walioombwa walishindwa. Kutokana na hali hiyo, kamati hiyo, kwa kushirikiana na Kamati ya Uongozi na Bodi, ilifanya uamuzi wa kuendelea na kongamano hata bila udhamini mwingine isipokuwa wa Chuo Kikuu cha Kibabii. Kuwepo kwa kongamano hili kunatokana na jitihada za kamati hiyo na kamati ya wenyeji iliyoongozwa na Dkt Fred Simiyu.

Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wanakamati wote kwa moyo wangu wote. Kamati kuu iliunda kamati ndogo tano: Kamati ya Mipango na Bajeti iliyoongozwa na Rais Dkt Filipo Lubua, Kamati ya Ikisiri na Ratiba iliyoongozwa na Dkt Peter Mwangi, Kamati ya Usajili na Uhamasishaji iliyoongozwa na Dkt Sarah Ngesu, Kamati ya Maslahi iliyoongozwa na Prof Mosol Kandagor na mwisho Kamati ya ununuzi wa bidhaa na huduma ambapo nilishirikiana na mhasibu Dkt Leonora Anyango, Prof. Leonard Muaka, Dkt Sarah Ngesu na Hezekiel Gikambi. Kamati hizi zilirahisisha sana mchakato.

Natoa shukrani za dhati kwa Chuo Kikuu cha Kibabii na hususani kwa Mkuu wa Chuo Prof Ipara kwa kukubali kuwa wenyeji wa kongamano hili la kumi la CHAUKIDU. Vilevile, naishukuru kwa mara ya pili kamati ya wenyeji, na haswa Mwenyekiti wake Dkt Simiyu, kutokana na kazi nyingi na muhimu walizofanya. Walijitolea kwa dhati. Pia nawashukuru wageni wetu waalikwa, kwa kukubali wito wetu. Pia, nawashukuru wageni wengine wote na kadhalika wale wote waliohusika katika kufanikisha kongamano hili.

Hatimaye, nawashukuruni washiriki wote mliotenga muda wenu kufika kwenye kongamano hili, ili tushirikiane katika kuerevushana katika nyanja mbalimbali zinazohusu akiliunde na lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Najua tuna washiriki kutoka sehemu nyingi za dunia, na wote wameletwa hapa na mapenzi yao kwa lugha ya Kiswahili. Natoa shukrani za dhati kwa wale waliowezesha warsha yetu hasa Rais Lubua na pia watoa mada kuu, Rais wa awali Dkt Mahiri Mwita na mwenzake katika Chuo Kikuu cha Princeton Happy Buzaaba.

Mwisho, naamini kwamba sote tutajifunza mengi katika kongamano hili. Ni matumaini yangu kwamba tutakayojifunza yatatufaa baadaye katika shughuli zetu za usomi na utafiti.

Ahsanteni tena na karibuni sana!

**Prof. Iribe Mwangi; PhD, MKNAS, HSC**
Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya

# Karibuni Chuo Kikuu cha Kibabii



**Fred Simiyu**

***Mwenyekiti, Kamati ya Wenyeji***

**NDUGU WAJUMBE,** WanaCHAUKIDU na wafia lugha ya Kiswahili,

Tuliyoyapanga kwa muda mrefu sasa yametimia. Nawakaribisheni sana hapa kwetu Chuo Kikuu cha Kibabii. Chuo Kikuu cha Kibabii kilizaliwa miaka kumi iliyopita. Kulingana na wenyeji wa eneo la Magharibi ya Kenya, neno 'Kibabii' linamaanisha *kurejea kwa mifugo zizini*. Maana hii ikizingatiwa kijazanda, inalandana na tija ya chuo hiki kwani ni mahali ambapo watu wa matabaka yote hukongamana kwa lengo la kupata maarifa na ujuzi. Kama njia mojawapo wa kuhuisha jina hili, tunawakaribisheni wakongamanaji kutoka kote ulimwenguni.

Ninaushukuru uongozi wa CHAUKIDU kwa kuchagua kuja Kibabii, lakini pia kuchagua mada faafu. Mada hii inalandana na falsafa ya Chuo Kikuu cha Kibabii ambayo inashikilia kwamba, ushirikishwaji wa sayansi, teknolojia na uvumbuzi ni nguzo muhimu sana katika kupata maendeleo endelevu pamoja na kujenga mazingira tulivu ya kufanya kazi.

Wakongamanaji wanakaribishwa sana katika chuo chetu, Chuo ambacho ni ngome ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Hapa chuoni, masuala ya Kiswahili yako chini ya Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, pamoja na Kituo cha Taaluma za Lugha na Utamaduni (CLACS). Chuo kimekuwa mstari wa mbele katika kupigania masuala ya Kiswahili. Kwa mfano, Kibabii ilikuwa mwenyeji wa Kongamano la CHAKITA la mwaka 2017. Aidha, chuo kimesherehekea mchango wa Ken Walibora katika Taaluma ya Kiswahili kwa kuendesha mihadhara ya umma ya kumuenzi Walibora kwa miaka miwili sasa. Kibabii pia kimeanzisha kona maalum ya vitabu vya Ken Walibora katika Maktaba ya Chuo pamoja na Makavazi ya Kitaifa ya Kitale. Juhudi hizi pamoja na nyingine zinaonesha msimamo wa chuo kuhusu Kiswahili. Hii ndio maana Kibabii walikubali bila kusita kuwa wenyeji wa kongamano hili la CHAUKIDU. Juhudi hizi zote za kutetea Kiswahili zilichochewa na ari pamoja na msukumo alio nao Makamu Mkuu mwanzilishi, Prof. Isaac Ipara Odeo. Ikumbukwe kwamba, Chuo Kikuu cha Kibabii kinaongozwa na mtaalamu bingwa wa Kiswahili. Huyu ni mtaalamu wa kwanza wa Kiswahili kuteuliwa kuwa makamu mkuu wa chuo kikuu nchini Kenya.

Nawashukuru sana viongozi wa Kamati Kuu ya CHAUKIDU wakiongozwa na Rais na wajumbe wa Kamati Andalizi ya Kongamano wakiongozwa na mwenyekiti wa Kamati, kwa kuhusika katika maandalizi ya Kongamano hili. Tumeshirikiana vizuri nao pamoja na kamati ndogondogo zilizoundwa kwa ajili ya kushughulikia masuala kadha wa kadha. Fauka ya hayo nawashukuru wenzangu waliokuwa katika Kamati ya Wenyeji: Dkt. Eric Wamalwa, Dkt, Gladys Kinara, Dkt. Mekarios Wakoko, Bw. Kelly Inyani, Bw. Meshak Nyambane na Bi. Deborah Kisongochi. Asanteni sana kwa ushirikiano wenu wakati wote wa kufanya maandalizi ya kongamano hili. Isitoshe, nawavulia kofia watoa mada, wawasilishaji, wakereketwa wa Kiswahili na washiriki wote ambao wamefanya maamuzi ya kushiriki kongamano hili. Ninaamini kabisa kwamba, kufikia mwisho wa kongomano hili tutakuwa tumechota hekima na maarifa kutoka kwa wakongamani wetu wanaokusanyika hapa Kibabii, kitovu cha makutano ya maarifa. Ninaamini kwamba, Kongamano hili litakuwa sehemu ya kumbukumbu ya kudumu kwa kila mmoja wetu. Karibuni sana Kibabii.

**Dkt. Fred, C. N. W. Simiyu,**

**Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya**

# RATIBA KWA MUHTASARI

## Siku 1 | Jumapili (14/12/2025)

| Saa | Shughuli |
|---|---|
| 2:45 Asb – 5:00 Asb | Usajili |
| 6:00 Mch – 11:00 Jio | Warsha |

## Siku 2 | Jumatatu (15/12/2025)

| Saa | Shughuli |
|---|---|
| 1:00 Asb – 2:50 Asb | Usajili na Matangazo |
| 3:00 Asb – 4:30 Asb | Vikao Sambamba 1 |
| 4:30 Asb – 5:00 Asb | Chai |
| 5:00 Asb – 6:25 Mch | Ufunguzi Rasmi |
| 6:25 Mch – 7:25 Mch | Makala Elekezi |
| 7:25 Mch – 7:50 Mch | Burudani na Picha |
| 7:50 Mch – 8:40 Mch | Chakula cha Mchana |
| 8:50 Mch – 9:50 Mch | Meza-Mduara: Sera, Wataalamu, na Wadau wa Kiswahili Katika Mapinduzi na Matumizi ya AI |
| 10:00 Jio – 11:30 Jio | Vikao Sambamba 2 |
| 11:30 Jio – 12:30 Jio | Kujumuika/Kutangamana + Chai ya Jioni |
| 12:30 Jio | Mapumziko ya Jioni |

## Siku 3 | Jumanne (16/12/2025)

| Saa | Shughuli |
|---|---|
| 1:30 Asb – 2:50 Asb | Usajili na Matangazo |
| 3:00 Asb – 4:30 Asb | Vikao Sambamba 3 |
| 4:30 Asb – 5:00 Asb | Chai |
| 5:00 Asb – 5:50 Asb | Makala Maalumu |
| 6:00 Mch – 7:30 Mch | Vikao Sambamba 4 |
| 7:30 Mch – 8:30 Mch | Chakula cha Mchana |
| 8:40 Mch – 10:00 Jio | Meza Mduara – Jukwaa la Lugha Zetu |
| 10:10 Jio – 11:10 Jio | Vikao Sambamba 5 |
| 11:10 Jio – 11:30 Jio | Kufunga Kongamano |
| 1:00 Usk – 6:00 Usk | Usiku wa Mswahili |

## Siku 4 | Jumatano (17/12/2025)

| Saa | Shughuli |
|---|---|
| 2:00 Asb – 11:00 Jio | Ziara ya Mji wa Bungoma na Viunga Vyake |

# AKILI IGE (AI) KAMA MTUMISHI MTIIFU

## KWA MWALIMU NA WANAFUNZI WA LUGHA

Warsha hii inachunguza namna AI inavyoweza kuwa mshirika mtiifu, makini, na mwenye kuleta ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Tutajadili mbinu sahihi za kuiingiza Akili Ige darasani ili kuongeza ubunifu, kuimarisha ufikivu wa rasilimali, na kuendeleza uwezo wa wanafunzi katika mawasiliano ya Kiswahili. Washiriki watapata mazoezi ya kivitendo.

**Filipo Gao Lubua**
*Mkurugenzi, Programu ya Lugha za Kiafrika*
*Chuo Kikuu cha Pittsburgh, Marekani*



Filipo Gao Lubua ana shahada ya uzamivu (Ph.D.) katika Teknolojia ya Ufundishaji (Instructional Technology) kutoka Chuo Kikuu cha Ohio kilichoko Ohio nchini Marekani. Kwa sasa, Filipo ni Profesa Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Pittsburgh, kilichopo mjini Pittsburgh, PA, Marekani, ambapo anafundisha kozi za Ujifunzaji Lugha kwa Msaada wa Kompyuta (ULUMKO). Pia anafundisha lugha na utamaduni wa Kiswahili na ndiye Mkurugenzi wa Programu ya Lugha za Kiafrika. Pia, Filipo ni Mhadhiri wa Kimuhula katika Chuo Kikuu cha Duquesne kilichoko hapohapo Pittsburgh. Katika Chuo Kikuu cha Duquesne, Filipo anafundisha kozi za Teknolojia ya Elimu (Instructional Technology) katika Ndaki ya Elimu chuoni hapo.

## USAJILI
## SAA 1:00 – 2:50 ASUBUHI

## HAKIKISHA UMEPITIA MEZA YA USAJILI NA KUPATA BEJI/KITAMBULISHO CHAKO

## VAA KITAMBULISHO CHAKO WAKATI WOTE WA KONGAMANO

| KISWAHILI | KIENEE |
| --- | --- |

# MBIU PRESS

**Mbiu Press®** ni chapa ya utetezi wa Mwafrika iliyodhamiria kuchapisha, kutunza na kusambaza kazi za Kiswahili zenye kuenzi historia, utamaduni na mchango wa Mwafrika katika fasihi na maarifa ya dunia. Jitihada hizi ni sehemu ya dira yetu ya kuhifadhi, kuenzi na kuene za maarifa na utamaduni wa Mwafrika kwa vizazi vya sasa na baadaye.

Mbiu press ndiye mchapishaji wa kazi za **Ebrahim Hussein**, **Penina Muhando**, **Euphrase Kezilahabi**, **Emmanuel Mbogo**, **Faraji Katalambula**, **MM Mulokozi**, **KK Kahigi**, **Mathias Mnyampala**, **FEMK Senkoro**, **Wilbard Makene** pamoja na mkusanyiko wa kazi za **Shaaban Robert**.

Kazi hizi zinapatikana katika mfumo wa nakala ngumu na nakala tepe (e-books) ili kuhakikisha kuwa zinawafikia kwa urahisi wasomaji wa Kiswahili duniani kote.




*Paza sauti ya Kiswahili*

**Mada: AI na Isimu/Isimu Tumizi ya Kiswahili**
**Mwenyekiti: Aidah Mutenyo**
**Mahali: ABB 015**

## MCHANGO WA AKILI MNEMBA KATIKA UFUNDISHAJI WA FONOLOJIA YA KISWAHILI

*Benitha France (Chuo Kikuu cha St. Augustine, Tanzania)*

Akili Mnemba (AI) ni uwanja unaounganisha isimu na teknolojia za kisasa katika kukuza matumizi ya lugha kidijitali. Hivyo, makala hii inachunguza mchango wa AI katika ufundishaji wa fonolojia ya Kiswahili. Utafiti huu umechunguzwa kupitia wataalamu mbalimbali kama vile Mazrui na Mazrui (1998), Hubbard na Levy (2006) pamoja na Nekoto na wenzake (2020) wanaodai kuwa uendelezaji wa lugha kiTEHAMA unategemea mchango wa AI kama fursa mpya ya kukuza lugha za Kiafrika. Uchunguzi wa utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi ya Noam Chomsky na Morris Halle (1968) na Nadharia ya Kujifunza kwa Mashine ya Arthur Samuel (1959). Lengo la utafiti huu ni kubaini mchango wa mifumo ya kujifunza Kiswahili kiotomatiki. Mbinu iliyotumika kukusanya data ni kusoma maandiko kuhusu fonolojia na ufundishaji wake kwa kutumia IA. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa AI inaweza kuchambua vipashio vya kifonolojia ndani ya maneno na kumsaidia mwanafunzi kuvibaini kupitia kusikiliza matamshi sahihi ya maneno hayo. Kadhalika, AI hutambua sauti hizo na kulinganisha na matamshi sahihi. Kwa hiyo, AI ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fonolojia ya Kiswahili kwani hurahisisha upatikanaji wa maarifa hata kwa wanafunzi walioko mbali au wanaojifunza mtandaoni.

## UCHANGANUZI WA SENTENSI YA KISWAHILI KWA KUTUMIA AKILIUNDE

*Fred Wanjala Simiyu (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Uchakataji Asilia wa Lugha unahusisha matumizi ya tarakilishi katika kupokea, kuchakata na kuzichanganua sentensi katika lugha. Kulingana na isimu ya Lugha ya Kiswahili, sentensi ndicho kipashio kikubwa miongoni mwa vipashio vya lugha ya Kiswahili. Aidha, sentensi huundwa kwa neno au fungu la maneno hivi kwamba hubeba taarifa kamili katika matini. Ili kuelewa muundo wa sentensi ya Kiswahili, uchanganuzi hutekelezwa kwa kutumia mikabala maalumu kutokana na aina zake. Makala hii inalenga kuchunguza jinsi akili unde inayoweza kutumika katika kuichanganua sentensi ya Kiswahili. Tunadhamiria kufafanua namna tarakilishi inavyoweza kupokea, kupanga na kuchambua sentensi ya Kiswahili katika programu za tarakilishi. Uchunguzi huu utaongozwa na nadharia ya Maana-Matini iliyoasisiwa na Zolk ˇ ovskij na Mel'ˇcuk (1965,1967). Nadharia hii inadai kwamba, katika uchakataji wa maana katika matini inayotolewa na mashine iwiane na maana asilia kwa mujibu wa wazawa wa lugha hiyo. Utafiti huu ni wa kithamano na utafanywa maktabani. Uchunguzi huu unadhamiria kuzidisha maarifa katika teknolojia ya lugha ya Kiswahili hususan ufafanuzi sarufi miundo ya Kiswahili kidijitali kwa kutumia akiliunde.

## UCHANGANUZI WA MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KATIKA MATUMIZI YA AI KATIKA TAHMNINI YA MASOMO YA ISIMU KWA WANAFUNZI WA KISWAHILI

*Mary Ndung'u (Chuo Kikuu cha Nairobi)*

Lugha ya Kiswahili imepitia mabadiliko makubwa katika uwanja wa Sayansi na Teknolojia. Kufikia sasa suala kuu la kiteknolojia ambalo limeipa Kiswahili mwamko mpya ni lile la matumizi ya akili-unde katika utafiti, ufundishaji, uchapishaji, utahini na hata katika mawasiliano. Hivyo basi utafiti huu unakusudia kuchunguza jinsi akili-unde inavyotumika katika tathmini. Ni dhahiri kwamba wanafunzi wamekuwa na utegemezi mkubwa katika mfumo wa akili unde ili kupata majibu ya maswali wanayoulizwa wakati wa mitihani. Mara nyingi wao hufanya hivyo kwa kujificha kwa kuwa sera ya chuo hairuhusu wanafunzi kurejelea matini zozote wakati wa mitihani. Wanastahili kurejelea kumbukumbu zao ili kupima uelewa wao katika somo fulani. Utafiti huu unalenga kuchunguza majibu yanayowasilishwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi katika mitihani ya Isimu hususan mitihani miwili ya kozi za Utangulizi wa Iismu na Mofolojia na Mofofonoljia ya Kiswahili. Katika kufanya hivyo, utafiti huu utachunguza kufanikiwa na kutofanikiwa kwa akili-unde katika kutoa majibu ya maswali ya kiisimu katika mitihani lengwa. Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (Corder, 1974). Data ya utafiti itakusanywa kutokana na majibu katika mitihani hii miwili

**Mada: Kiswahili AI na Lugha Nyingine za Kiafrika**
**Mwenyekiti: Beltha Ntanwa**
**Mahali: ABB 016**

## NAFASI YA AI KATIKA KUIFADHI LUGHA ZA KIAFRIKA/KIBANTU ZILIZOHATARINI KUTOWEKA NCHINI TANZANIA

*Muhtari Athumani (Chuo Kikuu Mzumbe)*

Tanzania ni nchi iliyopo katika bara la Afrika. Ni nchi yenye lugha za Kiafrika (Kibantu) zaidi ya 100. Kiswahili ni miongoni mwa lugha kati ya lugha za kibantu iliyopewa hadhi ya kuwa lugha ya taifa na kutengewa siku maalumu ya kuadhimishwa kimataifa. Wataalamu mbalimbali wamebainisha kwamba ijapokuwa ukuzaji wa Kiswahili ni jambo jema, kwa upande mwingine unadumaza jitihada za kuendeleza lugha nyingine za Kibantu nchini. Lugha nyingi za Kibantu nchini Tanzania zipo katika hatari ya kutoweka kutokana na hali ya kufifia kwa matumizi yake. Kwa hiyo, jitihada za kuhifadhi lugha hizo zinahitajika. Ni katika usuli huo, makala hii inaangazia nafasi ya AI katika kuhifadhi lugha za Kibantu za Tanzania. Data zitakusanywa kutoka kwa wataalamu 5 wa AI waliohitimu uga huo kwa ngazi ya shahada za uzamili. Lengo ni kupata namna bora ambayo AI inaweza kuhusika katika kuhifadhi lugha za Kibantu nchini Tanzania.

## NAFASI YA AKILI UNDE KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI NCHINI BURUNDI

*Sabushimike Ezéchias (Chuo kikuu cha Burundi)*

Akili Unde ni uwezo wa mashine au programu za kompyuta kuiga au kufanya kazi zinazohitaji akili ya binadamu. Katika mazingira ya kisasa ya kielimu, Akili Unde imekuwa nyenzo muhimu katika kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Aina hii ya teknolojia ya kisasa imebadilisha mambo mengi kwa kurahisisha kazi mbalimbali hasa kazi zinazohusiana na utafiti. Miongoni mwa kazi hizo, kuna ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kama vile Kiswahili. Nchini Burundi, Akili Unde hutumiwa na wanafunzi wa chuo kikuu kwa namna tofauti. Hata hivyo, changamoto kama vile ukosefu wa vifaa vya kiteknolojia na uhaba wa mafunzo kwa walimu na wanafunzi kuhusu matumizi ya Akili Unde zipo na zina athari katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Lengo la Makala hii ni kuchunguza jinsi akili unde inavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika chuo kikuu cha burundi pamoja na changamoto zinazojitokeza. Katika utafiti huu, tutatumia mbinu za hojji na mahojiano na kisha data zichambuliwe kwa kutumia majedwali na maelezo. Matokeo ya kazi hii yatakuwa muhimu katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kupitia ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia Akili Unde.

## NAFASI YA MAABARA YA LUGHA KAMA NJIA YA KUIMARISHA MATUMIZI YA AKILI-UNDE KATIKA MAFUNZO YA LUGHA KATIKA VYUO VIKUU

*Benard Odoyo Okal (Chuo Kikuu cha Maseno)*

Mafunzo ya masuala ya lugha yamebadilika kutokana na haja kubwa ya kuchanganya nyenzo anuwai za kiteknolojia ili kumsaidia mwalimu na mwanafunzi kuelewa dhana haraka au kufunza wanafunzi wengi kwa safari moja kwenye mitandao. Hali hiyo ya kuwepo na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia imechangia pakubwa uundaji wa nyenzo za kielektroniki na zisizo za kielektroniki zinazoweza kutumiwa darasani na katika maabara ya lugha. Vifaa vya kielektroniki ni nguzo muhimu ya kutuwezesha kuingiza programu au modeli za akili unde katika mafundisho ya masuala ya lugha. Hivyo basi, lengo kuu la makala haya ni kutathmini nafasi ya maabara ya lugha kama njia ya kuimarisha matumizi ya akili unde katika mafunzo ya lugha katika vyuo vikuu. Baadhi ya madhumuni ya kuongoza makala haya ni kama vile: kuchanganua aina za maabara ya lugha; kubainisha taipolojia za akili unde zinazoweza kutumiwa katika maabara ya lugha; na kuainisha aina za data zinazoweza kujumuishwa katika modeli za akili und

HAUKIDU
**Kwa Hisani ya**
**Chama Cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani**
**(CHAUKIDU)**

**Mada: AI na Lugha ya Kufundishia**
**Mwenyekiti: Mussa Hans**
**Mahali: ABB 0114**

## MITAZAMO YA WANAFUNZI WA KISWAHILI L2 KUHUSU MATUMIZI YA AKILI BANDIA (AI) KATIKA KUFUNDISHA NA KUJIFUNZA KISWAHILI

*Zelda Elisifa Sam (Chuo Kikuu Huria cha Tanzania)*

Utafiti huu unachunguza mitazamo ya wanafunzi wa Kiswahili L2 kuhusu matumizi ya teknolojia ya akili bandia (AI) katika kufundisha na kujifunza Kiswahili. Kwa kutumia nadharia ya Teknolojia ya Kukubalika (TAM) pamoja na mtazamo wa ujifunzaji wa ujengaji maarifa (constructivism), utafiti huu ulitumia mbinu mseto ambazo ni dodoso na mijadala ya vikundi kazi kutoka kwa wanafunzi 150 wa sekondari na vyuo vikuu vilivyoko Tanzania. Matokeo yanaonyesha kuwa wanafunzi wengi wana mtazamo chanya kuhusu matumizi ya akili mnembo, huku wakionesha kutambua manufaa yake katika kuboresha uandishi, msamiati, na upatikanaji wa rasilimali. Hata hivyo, baadhi yao walionesha wasiwasi mkubwa kuhusu ukosefu wa muktadha wa kitamaduni, utegemezi mkubwa, na uhaba wa zana za akili mnemba zinazotumia Kiswahili. Utafiti unapendekeza utengenezaji wa zana bunifu za akili mnemba zinazoakisi utamaduni wa Kiswahili pamoja na mafunzo ya uelewa wa kidijitali kwa walimu na wanafunzi.

## MITAZAMO YA WANAFUNZI KUHUSU AI KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI

*Moses Wamalwa Wasike (Chuo Kikuu cha Alupe ) & Cleophas Sikolia (Chuo Kikuu cha Kibabii )*

Ujio wa AI umebadilisha kwa kiasi kikubwa mbinu za ujifunzaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. Wanafunzi wengi hutumia AI kama wenzo wa kupata taarifa kwa ajili ya mijarabu, mijadala ya vikundi, na mawasilisho ya darasani. Licha ya mchango wake mkubwa katika elimu ya vyuo vikuu, mitazamo ya wanafunzi kuhusu wenzo huu haijabainishwa kwa kina. Mitazamo ya wanafunzi ni kipengele muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji kwani huwa ikichochea au kudhoofisha ari yao ya kujifunza. Kwa hivyo, walimu wanastahili kuipa kipaumbele darasani. Utafiti huu unalenga kuchunguza mitazamo ya wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya AI katika kujifunza Kiswahili. Nadharia ya Kukubalika kwa Teknolojia ya Davis (1986) itatumika kama mwongozo wa kinadharia. Utafiti utakuwa wa kimaelezo. Mbinu za utabakishaji na nasibu sahili zitatumika kuteua asilimia kumi ya vyuo na idadi sawa ya wanafunzi wa jinsia tofauti. Data itakusanywa kupitia hojaji na mahojiano, Hojaji zitaandaliwa kwa kuzingatia kiwango cha Likert. Data zitakazopatikana zitachanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia majedwali, grafu, na maelezo ya kina. Matokeo yanatarajiwa kufichua mitazamo na changamoto zinazowakumba wanafunzi wanapotumia AI. Hatimaye, utafiti utatoa mapendekezo ya mikakati itakayowasaidia walimu na watunga sera kuimarisha nafasi ya AI katika elimu ya vyuo vikuu nchini Kenya.

## CHANGAMOTO ZA AI KUELEWA MUKTADHA WA MAANA KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

*Mwanaisha Mohammed Omar (Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar)*

Katika karne 21 maendeleo ya Akili Bandia yameongeza kasi ya uchakataji lugha lakini bado kuna changamoto katika kuelewa muktadha wa maana katika Kiswahili. Utafiti huu umefanyika maktabani, umechunguza Mifumo ya AI ya kisasa kama ChartGpt na Geimin AI inavyoshungulikia tafsiri ya maana katika methali na misemo ya Kiswahili. Ingawa mifumo hii imeboreshwa, bado hutoa hutafsiri kwa njia ya moja kwa moja bila ya kuzingatia maana za kijamii na kiutamaduni. Mifumo hii Ina data finyu za Kiswahili na kushindwa kuhusisha maana na falsafa ya jamii. Utafiti huu umeongozwa na nadharia za zamani na sasa kama Pragmatiki leksia, Cultural linguistics (2017) kwa kusisitiza nafasi ya maarifa ya kiutamaduni. Transformer Deep language Models (2017) kama msingi wa ufasiri wa maana katika mfumo na Social Cultural Theory, inabainisha ujifunzaji hauwezi kutenganishwa na muktadha wa kijamii na kiutamaduni. Matokeo yamebainisha changamoto ya uhaba wa data, ukosefu wa kopra za kiutamaduni na ugumu wa kuiga uwelewa wa kijamii. Utafiti unapendekeza uundaji wa mifumo ya AI itakayofundishwa kupitia kopra pana za Kiswahili zenye maana ya kiutamaduni ili kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili.

**Mada: AI na Lugha ya Kufundishia**
**Mwenyekiti: Sarah Ngesu**
**Mahali: ABB 0115**

## FAIDA ZA KUTUMIA MAGAZETI KUFUNDISHIA KISWAHILI

*Nyabuto Choti (Chuo Kikuu cha Michigan State )*

Ufundishaji wa Kiswahili ng'ambo unakumbwa na tatizo la ukosefu wa vyanzo mwafaka. Ingawa, mtandao umeleta vyanzo vya kidijitali. Wasilisho hili litaangazia manufaa ya kutumia magazeti kufundishia Kiswahili. Mwandishi atarejelea kisa kimoja katika gazeti ta HabariLeo la Tanzania kujadili mada hii (Tanzania yatwaa ushindi wa kidijitali duniani). Kuna manufaa mengi ya kutumia magazeti kufundushia Kiswahili. Kwanza, hutoa mifano ya matumizi ya lugha katika miktadha halisi na kumwezesha mwanafunzi kujifunza msamiati, sarufi na misemo katika miktadha hiyo. Pili, huangazia utamaduni kama vile mitazamo, matatizo, itikadi, matukio, mila, desturi, na mijadala iliyoko katika jamii. Wanafunzi wanapata nafasi ya kulinganisha utamaduni wao na ule wa Waswahili. Tatu, hutoa istilahi za nyanja mbalimbali na zile zitumikazo kwa pamoja, k.m, michezo, siasa, na elimu. Nne, hutoa nafasi ya kujifunza kusoma na kwelewa mada tofauti za magazeti, k.m., habari, tahariri, maoni, na michezo. Pia, habari za magazeti zaweza kusomwa tena na kutumiwa kutayarisha maigizo na mazoezi ya kusoma, kusikiliza, kuzungumza, na kwandika. Tano, magaezti hubeba habari na matukio yanayojiri maishani mwa watu hivi sasa. Wanafunzi wana nafasi ya kusoma habari zinazowavutia, kutathimini matukio kwa kina, kutayarisha mijadala, miradi, mawasilisho, na maigizo. Mwisho, ni rahisi kupata magazeti kwenye mtandao na katika makitaba.

## TATHMINI YA MBINU ZA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA KISWAHILI IKIWA NI LUGHA YA KIGENI KWA KUTUMIA NADHARIATETE YA INGIZO

*Vinold John Mkenda (Chuo Kikuu cha St. Lawrence )*

Makala hii inachambua ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni kwa kuzingatia Nadharia ya Ingizo ya Steven Krashen. Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kumpatia mwanafunzi ingizo stahimilivu kwa kiwango chake cha uelewa ili kuwezesha ujifunzaji wa lugha mpya. Makala hii itatathmini matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia Nadharia ya Ingizo. Data zilipatikana kwa njia ya ushuhudiaji kutoka kwa walimu wanaofundisha Kiswahili kwa wageni. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kiwango cha maarifa mapya kinachoingizwa kwa mwanafunzi kinaathiriwa kwa kiasi kikubwa na mbinu zinazotumika. Aidha, utafiti ulibaini kuwa idadi kubwa ya walimu hutumia mbinu za ufundishaji bila kuzingatia kanuni za Nadharia ya Ingizo. Makala inapendekeza kuwa walimu wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni wapewe mafunzo maalumu kulingana na makundi na utofauti wa wanafunzi ili kudhibiti kwa ufanisi kiwango cha ingizo wanachowapa. Vilevile, mamlaka husika kama BAKITA, KIU na BAKIZA zinashauriwa kuandaa mitaala inayozingatia mbinu bora za ufundishaji na udhibiti wa kiwango cha ingizo katika kila somo, ili kuboresha ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni.

## AI, MAADILI, UTAMADUNI NA MAARIFA YA KIASILI

*Judy Onyancha (Chuo Kikuu cha Nairobi) na Rayya Timammy (Chuo Kikuu cha Nairobi)*

Katika kipindi hiki ambapo akili unde (AI) inatawala nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu, kuna haja ya dharura ya kuangazia nafasi ya lugha za Kiafrika — hasa Kiswahili — katika kuhifadhi, kuwasilisha, na kusambaza maadili, tamaduni, na maarifa ya jamii zetu. Makala hii inachunguza namna Kiswahili kinavyoweza kutumika kama nyenzo ya msingi katika kuhakikisha kuwa mifumo ya AI inajengwa kwa kuzingatia mazingira ya Kiafrika, na si kwa kufuata mifumo ya kiakili ya kigeni isiyoakisi mitazamo ya jamii zetu.Utafiti huu unachambua mifano ya matumizi ya Kiswahili katika programu za kutambua usemi, majukwaa ya elimu, na mifumo ya tafsiri kwa msaada wa mashine, ili kuonyesha jinsi maarifa ya kiasili na misingi ya kijamii inavyoweza kupotea au kupotoshwa endapo AI haitatengenezwa kwa muktadha wa lugha na tamaduni zetu. Aidha, makala inasisitiza umuhimu wa kushirikisha wataalamu wa Kiswahili, pamoja na wanazuoni wa fasihi, utamaduni na falsafa ya Kiafrika, katika upangaji wa sera na ubunifu wa teknolojia hizi. Kwa jumla, makala inapendekeza mikakati madhubuti ya kulinda utambulisho wa Kiafrika kupitia lugha, huku ikibainisha kuwa Kiswahili kina nafasi ya kipekee katika kufanikisha AI yenye maadili na mwelekeo wa Kiafrika.

## CHAI

## 4:30 ASUBUHI – 5:00 ASUBUHI
## UKUMBI MKUU – AUD C

## HAFLA YA UFUNGUZI RASMI

## 5:00 ASUBUHI – 6:25 MCHANA

## UKUMBI MKUU – AUD C

## MGENI RASMI

**Kenneth Inyani Simala**

***Profesa, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kenya***



Prof. Kenneth Inyani Simala ni msomi mtajika wa isimu na fasihi ya Kiswahili, ambaye kwa sasa ni Profesa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST), Kenya. Anaangazia masuala ya masomo ya Kiswahili, sera za lugha, na mijadala kuhusu tamaduni za Kiafrika. Simala ameandika na kuhariri kazi nyingi maarufu zikiwemo *Mitaala ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki* na *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya*. Akiwa Katibu Mtendaji Mstaafu wa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA), anahimiza matumizi ya lugha asilia kwa maendeleo endelevu na mshikamano wa kikanda.

## MWENYEKITI: PATRICK MOSE

Mahiri Mwita na Happy Buzaaba

# KUZIFUNZA KOMPYUTA KUELEWA LUGHA ZA KIAFRIKA





**Mahiri Mwita**
*Mhadhiri*
*Chuo Kikuu cha Princeton,*
*Marekani*

**Happy Buzaaba**
*Mhadhiri*
*Chuo Kikuu cha Princeton,*
*Marekani*

Makala elekezi inatoka kwa wataalamu wawili, Dkt. Mahiri Mwita na Dkt. Happy Buzaaba ambao wana mradi na kozi maalumu ihusianayo na AI, Modeli Kubwa za Lugha, yaani Large Language Models (LLMs), na Uchakataji wa Lugha Asilia (ULUA) yaani Natural Language Processing (NLP).

# JUMATATU 8:50 MCH – 9:50 MCH

***Meza Mduara – AUD C***

## MWENYEKITI



**Filipo Lubua**
*Chuo Kikuu cha Pittsburgh, Marekani*

## SERA, WATAALAMU, NA WADAU WA KISWAHILI

### KATIKA MAPINDUZI NA MATUMIZI YA AI



**Caroline Asiimwe**
*Katibu Mtendaji*
KAKAMA



**Consolata Mushi**
*Katibu Mtendaji*
BAKITA



**Leonard Muaka**
*Chuo Kikuu cha Howard*



**Saade Mbarouk**
*Mwenyekiti*
BAKIZA




**Patrick O. Mose**
*Chuo Kikuu cha Ohio*



**Iribe Mwangi**
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

## VIKAO SAMBAMBA NA. 2

## 10:00 JIONI – 11:30 JIONI




Tunawaalika wanachama na watafiti wote kuanza kutuma makala zao sasa ili ziweze kuchapishwa katika toleo lijalo. Hili ni jarida muhimu la kukuza tafiti, mawazo bunifu, na michango katika taaluma ya lugha na fasihi za Kiafrika.

**TUMA MSWADA WAKO SASA**

**MWENYEWE UTAFURAHI!**



**Mhariri Mkuu**

John Kiarie Wa'Njogu, Ph.D.
Chuo Kikuu cha Yale, Marekani

**KWA MASWALI**

Matbaa ya CHAUKIDU
2816 Cathedral of Learning
Pittsburgh, PA 15219
matbaa@chaukidu.org

**Mada: AI na Tafsiri/Ukalimani**
**Mwenyekiti: Michael Wairungu**
**Mahali: ABB 015**

## MATUMIZI YA AKILI UNDE KATIKA TAFSIRI YA KIINGEREZA KWENDA KISWAHILI: BARAKA AU BALAA?

*Mosol Kandagor (Chuo Kikuu cha Moi)*
*Fabiola Hassan (Chuo Kikuu cha Dodoma)*

Akili Unde imebadilisha mbinu za tafsiri kwa kujikita kwenye matumizi ya zana za kiotomatiki zinazoweza kushughulikia maandishi mengi kwa kasi ya juu. Hata hivyo, changamoto za kiisimu na kimuktadha, katika lugha za Kiafrika kama Kiswahili, zinahitaji uchunguzi ili kubaini ikiwa teknolojia hii ni baraka au balaa. Makala hii inafafanua faida za Akili Unde katika kuboresha upatikanaji habari pamoja na mapungufu yake katika kuhifadhi maana ya asili ya matini. Data zimetokana na uchambuzi wa matini 10 zilizotafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Matini hizi zilichaguliwa kwa usampulishaji lengwa wa kutegemea fursa. Ufasili wa data ulifanyika kwa mkabala wa kitaamuli, ambao unahusisha mbinu ya tathimini ya ubora na udhaifu wa tafsiri. Kuhusu ubora, makala inaonyesha kwamba Akili Unde inaweza kuwa baraka kwa kuongeza kasi, upatikanaji na ufanisi wa tafsiri. Kwa upande mwingine, Akili Unde ni balaa kwa sababu ya makosa ya kimantiki, upotevu wa maana ya kimuktadha na utegemezi wa kupindukia. Imehitimishwa kwamba ni muhimu kusawazisha faida na changamoto za matumizi ya Akili Unde. Aidha, imependekezwa kwamba zifanyike tafiti ili kuboresha mifumo ya Akili Unde ili kuongeza ufanishi wa tafsiri ya Kiingereza kwenda Kiswahili.

## ATHARI ZA MATUMIZI YA AKILI UNDE KATIKA UWANJA WA UTAFSIRI

*Bernard Oginga (Mfasiri Huru)*

Katika miaka miwili iliyopita, matumizi ya Akili Unde katika fani ya tafsiri yamebadilisha mahitaji ya wateja wa tafsiri. Kwa wastani, wafasiri wameripoti kwamba kazi za tafsiri zimepungua kwa asilimia 20. Hali hii imezua hofu miongoni mwa wafasiri wa Kiswahili kwamba kadiri mifumo mikubwa ya lugha (LLM) na akiliunde zalishi inavyozidi kuwa bora, ndivyo watakavyopoteza kazi. Hofu hii inatiliwa pondo na ukweli kuwa, tofauti na ilivyokuwa katika zama za matumizi ya tafsiri za mashine na uhariri wa tafsiri za mashine (MTPE), tafsiri zinazotokana na mifumo mikubwa ya lugha ni sahihi kwa asilimia kubwa ikilinganishwa na mifumo ya MTPE. Licha ya utafiti kuorodhesha fani ya tafsiri na ukalimani kuwa miongoni mwa zilizo na uwezekano mkubwa wa kupunguzwa na akiliunde, makala haya yatatalii fursa zilizopo na zilizoongezwa na akili unde kwa wafasiri, hasa wa Kiswahili. Miongoni mwa fursa hizo ni kushiriki katika kubuni akili unde zinazotegemea sauti badala ya kongoo za maneno.

## MATUMIZI YA AKILI UNDE KATIKA UTAFITI WA WANAFUNZI WA UZAMILI NCHINI UGANDA: HALI HALISI, FURSA, CHANGAMOTO NA MUSTAKABALI.

*Mutenyo Aidah (Chuo Kikuu Kabale)*

Kuongezeka kwa matumizi ya Akili Unde (AU) kumeibadilisha kwa kiasi kikubwa matazamo wa uzalishaji wa maarifa katika elimu ya juu, hususan miongoni mwa wanafunzi wa uzamili katika vyuo vikuu. Mabadiliko haya yamezua mjadala mpana kuhusu nafasi ya teknolojia katika mchakato wa utafiti. Makala hii inalenga kuchunguza matumizi ya AU katika utafiti wa wanafunzi wa Kiswahili wa uzamili katika vyuo vikuu vya Uganda, ikipima hali halisi, changamoto, na mustakabali wake. Uchunguzi unajikita katika hatua zote za utafiti, kuanzia kutafuta mada, kuandika mapendekezo, ukusanyaji na uchakataji wa data, uchambuzi wa takwimu na lugha, hadi uandishi na uwasilishaji wa matokeo. Pia, makala inatathmini fursa zinazotokana na matumizi ya AU, ikiwemo kuongeza ufanisi, kuboresha ubora wa uchambuzi, na kupanua upatikanaji wa rasilimali za kielimu vile vile kuonyesha changamoto kadhaa zinazoibuka, kama vile masuala ya uadilifu wa kitaaluma, utegemezi kupita kiasi wa teknolojia, upendeleo wa kimfumo, uvunjaji wa haki miliki, na ulinzi wa faragha ya washiriki wa utafiti. Matokeo yanayotarajiwa yanajumuisha mapendekezo ya sera na miongozo itakayoongoza vyuo vikuu katika kuweka misingi ya matumizi ya kuwajibika ya AU, kuwasaidia wasimamizi wa tafiti kuweka matarajio bayana, na kuwawezesha wanafunzi kutumia AU kama nyenzo ya kuongeza uwezo wa kiutafiti bila kudhoofisha fikra huru.

**Mada: AI na Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni**
**Mwenyekiti: Glady's Kinara**
**Mahali: ABB 016**

## MATUMIZI YA AI KATIKA KUTUNGA NA KUBORESHA MASOMO KWA WAGENI

*Mokaya Bosire (Chuo Kikuu cha Oregon)*

Katika mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni, mara nyingi walimu hulazimika kutumia muda wao mwingi katika kuandaa masomo kwa wanafunzi wao ikiwa ni pamoja na kutafuta picha, makala, matini, video na machapisho mengine mwafaka ya kufundishia hali halisi katika jamii lengwa ya Waswahili. Hili ni kwa sababu ya ukosefu wa raslimali hii mitandaoni na hasa katika vitabu vya kiada ambavyo vinaweza kutumika kwa kazi hii. AI inaweza ama kukarabati matini zilizopo au kubuni matini na picha kwa matumizi ya darasani kwa haraka na kulingana na matakwa ya darasa na mwalimu wake. Katika wasilisho hili tutajadili na kuchambua baadhi ya njia AI inavyoweza kutumika kama chombo cha kufundishia na kuauni walimu wa lugha na kuboresha zaidi mafunzo ya utamaduni wa lugha lengwa."

## ATHARI ZA AI KATIKA UFUNDISHAJI WA KISWAHILI KWA WAGENI

*Patrick Oyinda (Chuo Kikuu cha Howard)*

Ufundishaji Kiswahili kwa wageni ni mchakato unaopaswa kutekelezwa kwa umakini. Kiswahili ni lugha inayozidi kusambaa na kukumbatiwa na mataifa mengi duniani. Hivi sasa, kunashuhudiwa ongezeko la idadi ya wanafunzi kutoka pembe mbalimbali duniani na ambao wana ari kubwa ya kujifunza Kiswahili. Hali kama hii ni ishara ya kuwepo kwa mustakabali mng'avu wa Kiswahili. Hata hivyo, tunaishi katika karne ambayo teknolojia inazidi kuvumbuliwa na kukua kwa kasi sana. Isitoshe, binadamu wamo mbioni kuonyesha ubunifu wao katika matumizi ya teknolojia ili kurahisisha mambo mbalimbali katika mazingira wanamoishi. Hali hii imesababisha wasomi, wakiwemo baadhi ya wageni wanaojfunza Kiswahili, kutumia akili mnemba (AI) ili kurahisisha mchakato wao wa ujifunzaji lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, makala hii inalenga kutambua athari za matumizi ya AI katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni na kupendekeza mikakati faafu ili kufanikisha ukamilifu wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wake kwa wageni. Data ya utafiti huu itapatikana kwa kutumia mbinu za mahojiano na hojaji. Data inayolengwa ni stahilifu na itachanganuliwa kwa njia ya maelezo ya kina kwa kuzingatia mada na malengo ya utafiti huu. Watafitiwa watakaoshirikishwa watachaguliwa kwa njia ya kimaksudi. Nadharia ya jamii na tamaduni ya Vygotsky itatumiwa katika uchanganuzi wa data.

## MITAZAMO YA WANAFUNZI KUHUSU AI KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI

*Moses Wamalwa Wasike (Chuo Kikuu cha Alupe ) & Cleophas Sikolia (Chuo Kikuu cha Kibabii )*

Ujio wa AI umebadilisha kwa kiasi kikubwa mbinu za ujifunzaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. Wanafunzi wengi hutumia AI kama wenzo wa kupata taarifa kwa ajili ya mijarabu, mijadala ya vikundi, na mawasilisho ya darasani. Licha ya mchango wake mkubwa katika elimu ya vyuo vikuu, mitazamo ya wanafunzi kuhusu wenzo huu haijabainishwa kwa kina. Mitazamo ya wanafunzi ni kipengele muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji kwani huwa ikichochea au kudhoofisha ari yao ya kujifunza. Kwa hivyo, walimu wanastahili kuipa kipaumbele darasani. Utafiti huu unalenga kuchunguza mitazamo ya wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya AI katika kujifunza Kiswahili. Nadharia ya Kukubalika kwa Teknolojia ya Davis (1986) itatumika kama mwongozo wa kinadharia. Utafiti utakuwa wa kimaelezo. Mbinu za utabakishaji na nasibu sahili zitatumika kuteua asilimia kumi ya vyuo na idadi sawa ya wanafunzi wa jinsia tofauti. Data itakusanywa kupitia hojaji na mahojiano, Hojaji zitaandaliwa kwa kuzingatia kiwango cha Likert. Matokeo yanatarajiwa kufichua mitazamo na changamoto zinazowakumba wanafunzi wanapotumia AI. Hatimaye, utafiti utatoa mapendekezo ya mikakati itakayowasaidia walimu na watunga sera kuimarisha nafasi ya AI katika elimu ya vyuo vikuu nchini Kenya.

**Mada: AI na Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni**
**Mwenyekiti: Rayya Timammy**
**Mahali: ABB 0114**

## AKILIUNDE NA UFUNDISHAJI WA FASIHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI NCHINI KENYA

*Sarah Ngesu (Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya)*
*Justus Saboe Makhokha (Chuo Kikuu cha Kenyatta)*

Utafiti ulichunguza matumizi ya Akiliunde (AI) katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili kwenye shule za sekondari nchini Kenya. Licha ya ukwasi wa fasihi ya Kiswahili, mbinu za ufundishaji zimeendelea kuwa za kawaida, jambo ambalo limepunguza motisha na uelewa wa wanafunzi. Nadharia ya Kujifunza kwa Kujenga iliongoza uchanganuzi wa data. Mbinu za hojaji, mahojiano na ushuhudiaji zilitumika kukusanya data. Sampuli ya watoataarifa 100 kutoka shule za umma na za binafsi katika kaunti teule walihusishwa. Data zilichanganuliwa kitakwimu na kitaamuli. Matokeo yanaonesha kuwa zana za AI kama vile majukwaa ya kujifunza ya kiutangamano, tafsiri na uchambuzi wa maandishi kiotomatiki na programu za usindikaji lugha, zikuza motisha na uelewa wa wanafunzi. Hata hivyo, ufundishaji huu ulikumbwa na changamoto za miundombinu ya teknolojia na upungufu wa mafunzo ya AI kwa walimu.

## AI NA UHIFADHI WA LUGHA ZA KIASILI

*Andrew Watuha (Chuo Kikuu cha Nairobi)*

Akili Mnemba inachangia pakubwa katika uhifadhi na uhamasishaji wa lugha za asili ambazo zinakabiliwa na hatari ya kutoweka kutokana na kupungua kwa idadi ya wazungumzaji na athari za ulimwengu. Kwa kutumia Akili Mnemba, zana bunifu zinaweza kuundwa ili kurekodi, kufundisha, na kuhamasisha lugha hizi, kuhakikisha kuendelea kwazo kwa vizazi vijavyo. Mchango mkuu utakuwa katika kuratibu lugha, ambapo zana za Akili Mnemba zinasaidia katika kurekodi, kuandika na kuachanganua lugha za asili. Mifumo ya kiotomatiki ya Akili Mnemba inaruhusu uhifadhi wa Fasihi simulizi na hadithi za kijamii ambazo ni kitambulisho cha utamaduni. Zaidi ya hayo, Akili Mnemba inaimarisha majukwaa ya kujifunzia lugha kibinafsi au kwa kushirikiana. Aidha, tafsiri ya mashine inayoendeshwa na Akili Mnemba inaimarisha mawasiliano na kubadilishana kwa tamaduni. Baadhi ya lugha za asili duniani tayari zimefaidika na maendeleo haya, zikionyesha uwezo wa Akili Mnemba katika kuimarisha lugha hizi kama turathi. Karatasi hii inalenga kuchunguza njia mbalimbali ambazo Akili Mnemba inaweza kutumika kusaidia katika uhifadhi na uhamasishaji wa lugha za asili, ikisisitiza utekelezaji uliofanikiwa, changamoto na athari kwa ustawi wa lugha za asili katika miaka ijayo.

## UFASILI NA UPAMBANUZI WA KIRAI NA KISHAZI CHA KISWAHILI: TATHMINI YA HABARI ZA CHATGPT

*David Masinde Wanyonyi (Chuo Kikuu cha Moi)*
*Mosol Kandagor (Chuo Kikuu cha Moi)*

Baadhi ya wataalamu, wametoa tetezi kuihusu isimu ya lugha ya Kiswahili. Baadhi yao husema, isimu ya lugha ya Kiswahili ni ngumu ukilinganisha na fasihi ya Kiswahili, sintaksia ndiyo ngazi ngumu sana kuliko ngazi zingine za isimu kama, fonolojia, mofolojia na semantiki (Mathooko, 2002). Imegunduliwa kuwa kuna utata na uchangamano fulani kwenye ufasili na upambanuzi wa virai na vishazi vya lugha ya Kiswahili kwenye baadhi ya vitabu vya msingi vya sintaksia ya Kiswahili (Masinde, 2023). Matumizi ya akiliunde yamepanuka na haiepukiki katika maisha ya kisasa. Teknolojia ya akiliunde imerahisisha mambo, kwa kusaidia katika utoaji wa uamuzi, ujifunzaji na maendeleo, kuboresha tajriba, kusaidia kupunguza hatari, kwa, uwezo na uamilifu kwa kukabili hali mabalimbali (ChatGPT). Kuwepo kwa teknolojia ya akiliunde, kuliwachochea watafiti kuchanganua virai na vishazi vya lugha ya Kiswahili vilivyofasiliwa na kupambanuliwa katika ChatGPT kwa nia ya kutaka kutambua iwapo pia kuna utata na uchangamano. Utafiti uliongozwa na baadhi ya mihimili ya nadharia ya X-BAA na ya Mifumo. Imechukuliwa kuwa matokeo na mapendekezo ya uchunguzi huu yatakuwa ya manufaa hasa kwa wataalamu wa sintaksia ya lugha ya Kiswahili wanaohusika na akiliunde

**Mada: AI, Fasihi, na Sanaa ya Kiswahili**
**Mwenyekiti: Vinold Mkenda**
**Mahali: ABB 0115**

## MCHANGO WA AI KATIKA UTATHMINI WA MAARIFA ASILIA YA KIAFRIKA: MFANO KUTOKA RIWAYA YA KISWAHILI

*Naomi Musembi (Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga), Peter Karanja (Chuo Kikuu cha Gretsa), & Fred Simiyu (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Makala hii inadhamiria kuangazia mchango wa AI katika utathmini wa maarifa asilia ya Kiafrika. Utafanya hivyo kwa kutathmini riwaya ya Walenisi ya G.K. Mkangi. Madhumuni ya makala hii ni kutanua mchango wa AI katika fasihi andishi hasa riwaya ya Kiswahili katika kuangazia maarifa asilia ya Kiafrika na jinsi maarifa hayo yanavyoweza kumkomboa Mwafrika dhidi ya matatizo anayokumbana nayo kila uchao. Ikiongozwa na nadharia ya Ujumi mweusi hasa mhimili unaosisitiza umuhimu wa mwonoulimwengu wa Kiafrika katika kufanikisha maendeleo ya Mwafrika, makala hii inahoji kuwa, ili fasihi iwe na manufaa kwa jamii, ni lazima iwe chombo kiaminifu cha jamii hiyo. Ni lazima iwe na jukumu la kueleza, kuchambua, kukosoa na kuongoza jamii.

## MCHANGO WA AI KATIKA KUKUZA NA KUENDELEZA FASIHI YA WATOTO

*Rose Mavisi (Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki)*

Kutokana na maendeleo makubwa ya kiteknolojia duniani, Akili Unde(AI) imeanza kupewa nafasi katika nyanja mbalimbali za maisha, ikiwemo sekta ya elimu na sanaa. Teknolojia ni pumzi ya ulimwengu katika karne ya 21 kwa sababu inaendesha shughuli nyingi za binadamu (Gikambi, 2003). Nchini Kenya, fasihi ya watoto imekuwa ikikua kupitia mbinu za jadi kama vile simulizi za mdomo, na uchapishaji wa vitabu. Hata hivyo, kuibuka kwa AI kumeleta fursa mpya za ubunifu. Changamoto iliyopo ni kuelewa kwa kina jinsi AI inavyoweza kutumika ipasavyo kukuza fasihi ya watoto bila kuathiri ubunifu wa kibinadamu. Aidha, bado kuna upungufu wa tafiti zinazochunguza nafasi ya AI katika kutunga na kuhifadhi kazi za fasihi ya watoto nchini Kenya. Hali hii inahitaji uchunguzi ili kubaini mchango wa matumizi ya AI katika kukuza fasihi ya watoto nchini Kenya. Utafiti huu utalenga kuchunguza mchango wa teknolojia ya Akili Unde katika kukuza na kuendeleza fasihi ya watoto katika mazingira yanayobadilika ya maandishi ya kidijitali. Utafiti huu utatumia muundo wa kitaamuli katika ukusanyaji wake wa data. Mtafiti atasoma makala na vitabu maktabani ili kudondoa data inayohitajika.

## UMUHIMU WA AKILI UNDE KWA KUIMARISHA BIASHARA YA SANAA HASA KWA WASANII WA MUZIKI, KUIGIZA, NA WACHESHI

*Anna Mwalagho (Chuo Kikuu cha Howard )*

Akili mnemba au Akili unde, ni teknologia ambayo inautata na ina mashabiki na pia maaadui. Katika maswala ya kuajiriwa, watu wengi wanaamini kuwa akili unde, ina chukua nafasi zao za kazi, na basi wana hofu sana na teknologia hiyo. Lakini kwa wale wasanii au wanasanaa, akili unde, inaonekana kuleta faida sana kwa kupunguza gharama ya kutengeneza video za muziki, vipande vidogo ya kuigiza, vichekesho vya televisheni,, filamu, na video za mitandao ya jamii. Hasa kwa wasanii walioko na bajeti dogo na wangependa kuendeleza biashara zao za kisanii, kufahamu na kuelewa jinsi ya kutumia akili unde ni jambo la busara sana. App kama Capcut, imovie, concerge AI, ChatGPT na kadhalika zina weza kurahisisha kazi za msanii yoyote na pia kuendeleza ujuzi na biashara au umaarufu wa msanii. Nitachukua fursa, hii katika kongamano hili kufunza wadau jinsi ya kutumia app hizi , na manufaa ya akili unde katika maisha ya msanii au katika sanaa.

# RATIBA KWA MUHTASARI
# JUMANNE TAREHE 16

| Saa | Shughuli |
|---|---|
| 1:30 Asb – 2:50 Asb | Usajili na Matangazo |
| 3:00 Asb – 4:30 Asb | Vikao Sambamba 3 |
| 4:30 Asb – 5:00 Asb | Chai |
| 5:00 Asb – 5:50 Asb | Makala Maalumu |
| 6:00 Mch – 7:30 Mch | Vikao Sambamba 4 |
| 7:30 Mch – 8:30 Mch | Chakula cha Mchana |
| 8:40 Mch – 10:00 Jio | Meza Mduara – Jukwaa la Lugha Zetu |
| 10:10 Jio – 11:10 Jio | Vikao Sambamba 5 |
| 11:10 Jio – 11:30 Jio | Kufunga Kongamano |
| 1:00 Usk – 6:00 Usk | Usiku wa Mswahili |

**Kwa Hisani ya**
**Chama Cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani**
**(CHAUKIDU)**


CALLiT Africa
We Bring Your Global
Learning Vision to Life
Our programs are:
Flexible and responsive to your needs
Academically aligned
Culturally immersive
CALLiT
AFRICA
Computer-Aided Lasting Learning
Find us in Tanzania and Kenya.
We've Partners all over Africa.
At CALLiT Africa,we design customized study abroad programs that match the goals of both students and instructors. Whether you're seeking culture - rich academic immersion, outdoor experiential learning, or faculty-led travel courses, we make it happen.
Partner with us to co-create a transformative African learning journey tailored just for your group
CALL NOW
+255 762 448 403
director@callitafrica.com
www.callitafrica.com
PANDA

**Mada: AI, Fasihi, na Sanaa ya Kiswahili**
**Mwenyekiti: Flora Malema**
**Mahali: ABB 015**

## AI NA UFUNZAJI WA KOZI YA FASIHI KATIKA VYUO VIKUU NCHINI KENYA: MFANO WA CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA KOITALEEL SAMOEI

*Priscah Jebet Kiprotich (Chuo Kikuu Kishiriki cha Koitalel Samoei)*

Matumizi ya programu za akili unde mfano wa chatGPT katika kukamilisha mazoezi ya uhakiki wa fasihi miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu yamesababisha matokeo bora au duni kwenye kozi za fasihi. Hali hii inazua haja ya utafiti ili kubaini njia bora za kujumuisha akili unde katika ufunzaji na ujifunzaji wa kozi za fasihi vyuoni. Makala yanalenga kuonyesha mchango wa programu ya chatGPT katika ufunzaji wa fasihi kwenye vyuo vikuu nchini Kenya. Utafiti huu wa kimfano utawalenga wanafunzi wa fasihi ya kiswahili kwenye chuo kikuu kishiriki cha Koitaleel Samoei. Ili kutimiza lengo kuu la utafiti, mtafiti atajaribu kujibu maswali matatu: wanafunzi wa vyuo vikuu wanazingatia vigezo vipi wanapotumia chatGPT katika kuhakiki kazi za fasihi? Manufaa ya chatGPT katika uhakiki wa kazi za fasihi ni yapi na upungufu wa chatGPT katika uhakiki wa kazi za fasihi ni upi? Utafiti huu unahimiza hasa wanafunzi na wahadhiri wa fasihi kupewa maarifa zaidi ya matumizi ya akili unde katika elimu. Usampulishaji wa kimatilaba utatumiwa ili kulenga tu kozi za fasihi ya kiswahili. Data itakusanywa kupitia mahojiano.

## NAFASI YA HADITHI ZA KIHA KATIKA JAMII YA VIJANA KATIKA ULIMWENGU WA AI.

*Olivia Kanwa (Chuo Kikuu cha Bishop Stuart )*

Licha ya kuwepo kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia bado tanzu za kifasihi simulizi zikiwemo hadithi zinaheshimiwa katika jamii nyingi za Kiafrika kwa kuwa zinatumika kuhifadhi historia na kuendeleza amali za jamii. Kutokana na umuhimu wa hadithi hizo katika jamii, makala hii imechunguza nafasi ya hadithi za Kiha katika jamii ya vijana katika ulimwengu wa AI. Makala imeongozwa na malengo mahususi matatu ambayo ni : kubainisha hadithi zinazotumiwa na Waha katika wilaya ya

Kasulu kata ya Nyamidaho, kueleza dhima ya hadithi za Kiha katika jamii ya vijana wa Kiha pamoja na ujumbe uliomo katika hadithi hizo na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kudumisha hadithi hizo. Nadharia ya usosholojia ya fasihi ambayo imemwongoza mtafiti kuzikusanya hadithi mbalimbali na kuzichambua na nadharia ya utendaji wa maigizo imemwezesha mtafiti kuutambua utendaji miongoni mwa hadhira na tabia zao. Mtafiti alitumia usampulishaji wa makusudi na wa kubahatisha ili kuweza kupata sampuli iliyosaidia kutoa taarifa zilizohitajika kuhusu nafasi ya hadithi za Kiha katika jamii ya vijana katika ulimwengu wa sasa wa AI. Kupitia mbinu ya mahojiano, hojaji, ushiriki na ushuhudiaji kwa kutumia vifaa mbalimbali ili kupata taarifa zinazohitajika.

## MATUMIZI YA AI KATIKA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA PILI

*Anyonje Florence (Chuo Kikuu Kishiriki cha Bomet).*

**Mada: AI, Maadili, Utamaduni, na Maarifa ya Kiasili**
**Mwenyekiti: Mosol Kandagor**
**Mahali: ABB 016**

## MATUMIZI YA AI KATIKA UHUISHAJI WA NGANO MIONGONI MWA BABUKUSU

*Betty Nasambu (Chuo Kikuu cha Kibabii), Fred Wanjala Simiyu (Chuo Kikuu cha Kibabii)*
*Gladys Kinara (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Hadithi za Jadi za Wabukusu kihistoria zimetumika kama zana muhimu za kusambaza maadili, kanuni za kijamii na utambulisho wa kitamaduni katika jamii za Magharibi mwa Kenya. Hata hivyo, mabadiliko ya haraka ya kisasa na udijitalishaji imesababisha kupungua kwa uwasilishaji wa simulizi za hadithi hizi, na kujenga pengo la kitamaduni kati ya vijana na wazee. Makala hii inalenga kuchunguza jinsi kuwekwa kwa ngano za Bukusu kwenye fomati za kidijitali kama vile video, podikasti, na programu za rununu kutaweza kukuza maadili na uhifadhi wa utamaduni. Makala hii itaongozwa na Nadharia ya Uamilifu iliyoasisiwa na wanasosholojia Auguste Comte, Harbert Spencer Vilfredo na Emile Durkheim na baadaye kuendelezwa na mwana anthropolojia Radcliffe Brown na Malinowski Malinowski (Wallance na Wolf, 1980). Mbinu ya uchunzaji mahuluti itatumika kusanya data hitajika. Utafiti utatumia sampuli madhubuti kutambua watoa taarifa muhimu kama vile wazee wa kitamaduni na sampuli kimkakati kuchagua vijana kuhakikisha uwakilishi mbalimbali. Data itachanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaelezo.

## MCHANGO WA AKILI UNDE KATIKA KULINDA, MAADILI YA JAMII, UTAMADUNI NA MAARIFA YA KIASILI

*Saade Said Mbarouk (Baraza la Kiswahili la Zanzibar)*
*Mwanahija Ali Juma (Baraza la Kiswahili la Zanzibar)*

Kuna istilahi nyingi zinazotumika kubainisha kisawe Artificial Intelligence (AI); maneno kama vile akili unde, akili mnemba na akili bandia yametumika. Katika makala hii tutatumia istilahi akili unde, hata hivyo tutakaponukuu tutamia istilahi tuliyoinukuu kitabuni. Akili bandia ni mchakato wa kuifundisha mashine ili ifikiri na itende kama mwanadamu. Anaendelea kueleza kuwa akili bandia ni teknolojia inayomwezesha mashine kujifunza, kufikiri na kutenda kama mwanadamu. Anasisitiza kueleza kuwa hizi ni juhudi za wanadamu kuipatia mashine uwezo wa kufanya maamuzi bila uhitaji wa mtu kuiendesha moja kwa moja. Akiliunde ni nyenzo katika kuhifadhi na kukuza maadili ya yamii, utamaduni, na maarifa ya kiasili. Kwa kutumia mbinu za kisasa za kidijitali teknolojia hii inawezesha ukusanyaji,uhifadhi na usambazaji wa taarifa za kitamaduni na maarifa ya jamii kwa urahisi na usahihi mkubwa. Katika makala hii, tunajadili mchango wa AI katika kulinnda urithi wa utamaduni, kujenga mifumo inayoheshimu maadili ya kijamii na kusaidia uendelevu wa maarifa ya kiasili. Katika makala hii tutatumia nadharia za Ethics – Based AI na Nadharia ya Uhifadhi wa Utamaduni. Aidha, mifano ya kitaifa na kimataifa inayoonesha jinsi AI inavyotumika kulinda lugha, mbinu za tiba asilia, na utambulisho wa jamii zitabainishwa.

## SAFARI ZA KISWAHILI: KUJIFUNZA LUGHA NA KUJENGA USHIRIKIANO KATIKA MASOMO YA UGHAIBUNI

*Michael Wairungu na Vinold Mkenda (Chuo Kikuu cha St. Lawrence)*

Walimu wengi walio katika hatua za awali za taaluma zao katika Ughaibuni, hususan wale wanaofundisha lugha na tamaduni za Kiafrika, mara nyingi hutamani kuandaa programu za masomo ughaibuni (study abroad) kama vile Afrika Mashariki, lakini kwa kawaida hawajui waanzie wapi. Hata wale walio na mawazo yaliyo wazi kuhusu maeneo ya kuwapeleka wanafunzi wao hukosa washirika wa kuwasaidia kushughulikia masuala muhimu kama vile mada ya kitaaluma, usalama, idhini ya serikali, usafiri, masuala ya afya na ushauri nasaha, pamoja na "wataalamu" wa tamaduni za wenyeji. Katika uwasilishaji huu, tunalenga kujibu maswali hayo na mengine zaidi kwa kueleza Programu ya Muhula ya Chuo Kikuyu cha St. Lawrence inayofanyika nchini Kenya. Tutaonesha uzoefu wa programu, kozi zinazotolewa, pamoja na uhusiano wa kina kati ya madarasa yetu ya lugha ya Kiswahili na vipengele vya mafunzo ya uwandani. Hatimaye, tunatarajia kuwashirikisha washiriki wa kongamano la CHAUKIDU katika mjadala unaoangazia uhusiano kati ya ufundishaji wa darasani na utekelezaji wa mafunzo kwa vitendo uwandani. Pia tunasisitiza umuhimu wa kushirikiana na taasisi zenye uzoefu mkubwa wa kuendesha programu za masomo ughaibuni, kama Programu ya Chuo Kikuu cha St. Lawrence Nchini Kenya

**Mada: AI, Teknolojia, na Ukuzaji wa Kiswahili**
**Mwenyekiti: Muhtari Athmani**
**Mahali: ABB 0114**

## UTATHMINI WA MATUMIZI YA AI KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI

*Hamisi Babusa (Chuo Kikuu cha Kenyatta)*

Kuibuka kwa teknolojia ya Akili Unde (AI) kumebadilisha mazingira ya kimawasiliano, kiuchumi, na kielimu kwa kiwango kikubwa duniani kote. Katika nyanja ya elimu, AI imeanza kutumika si tu kama nyenzo ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu, bali pia kama mwezeshaji wa mbinu shirikishi na bunifu za kujifunza na kufundisha. Makala hii inajikita katika kuchunguza matumizi ya AI katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Madhumuni ya makala hii ni matatu; kutathmini matumizi ya AI katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, kubainisha ufaafu wa matumizi ya AI katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, kuainisha udhaifu wa matumizi ya AI katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Makala yataelekezwa na nadharia ya Ujifunzaji wa Kijamii iliyoasisiwa na mwanasaikolojia Albert Bandura katika miaka ya 1960, inayosisitiza kujifunza kwa mwingiliano baina ya mwanafunzi, mwalimu na mazingira. Kwa kutumia mbinu ya maktabani na uchambuzi wa mifano ya matumizi ya AI katika lugha nyingine, makala hii itatoa mapendekezo ya namna ufundishaji na ujifunzajo wa Kiswahili unavyoweza kufanikishwa na matumizi ya AI.

## FILAMU YA EX MACHINA: MAANA NA MAUDHUI YAKE KATIKA MATUMIZI YA AI

*Leonora Anyango (Chuo Kikuu cha Pittsburgh)*

Katika ulimwengu unaozidi kuwa na teknolojia zinazoendelea kwa kasi, AI ni kama taa ya maendeleo na pia ishara ya hofu. Filamu kwa muda mrefu zimekuwa na jukumu muhimu katika kufafanua jinsi jamii inavyochukulia AI- si tu kama mashine zenye uwezo wa kujifunza, bali kama viumbe vinavyotishia kuzidi akili ya binadamu, uhuru na maadili. Taswira hii inafichua mahangaiko ya ndani ya jamii kuhusu kupoteza udhibiti, mipaka ya kimaadili, na mustakabali usiojulikana wa ubinadamu. Katika Ex Machina (2014), mkurugenzi Alex Garland anarejelea hofu hizi kwa kubuni simulizi ya kusisimua ambapo AI hupata hisia na kumdanganya muundaji wake. Kupitia matumizi yake ya kimakusudi ya mpangilio, mazungumzo, na mienendo ya wahusika, Garland anaonyesha wasiwasi wetu kuhusu kuongezeka kwa AI. Ni dhahiri kwamba filamu kama Ex Machina haziburudishi tu- ni kama kioo kwa hofu zetu juu ya AI. Kwa kurejelea filamu hii na maudhui yake, wasilisho hili litafafanua jinsi ambavyo sisi kama waalimu wa Kiswahili tunaweza kuwa na wasiwasi juu ya AI na matumizi yake katika kazi zetu. Tutajadili zaidi juu ya filamu hii na jinsi ambavyo inaweza kutufundisha juu ya AI na matumizi yake katika kazi zetu.

## NAFASI YA AKILI MNEMBA KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI

*Sarah Vincent (Chuo Kikuu cha Dodoma)*

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameibua mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika katika ujifunzaji wa lugha. Ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni nao umeanza kunufaika na maendeleo haya ya kiteknolojia. Makala hii inachambua nafasi ya akili mnemba katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni, ikiangazia umuhimu na changamoto. Data za makala hii zimekusanywa kwa njia ya mahojiano na uchambuzi matini na kuchanganuliwa kitaamuli. Aidha, nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Vygotsky (1978) inayosisitiza mwingiliano wa kijamii katika ujifunzaji wa lugha imetumika. Matokeo ya utafiti wa makala hii yameonesha kuwa matumizi ya akili mnemba yana mchango katika kuongeza hamasa na kurahisisha ujifunzaji. Aidha, imebainika kuwa zipo changamoto za matumizi ya akili mnemba katika ujifunzaji ambazo ni kukosekana kwa programu za akili mnemba zilizo sanifu na mahususi kwa lugha ya Kiswahili, jambo linalodhoofisha ufanisi wa ujifunzaji kwa kutumia teknolojia hii. Makala hii inapendekeza kuwa, ingawa akili mnemba ni nyenzo muhimu, bado kunahitajika jitihada za pamoja kuhakikisha matumizi yake yanalingana na muktadha wa kitamaduni, kijamii, na kiisimu wa lugha ya Kiswahili.

**Mada: AI, Utafiti na Uchapishaji, Habari na Magazeti**
**Mwenyekiti: Gordien Ndayikengurukiye**
**Mahali: ABB 0115**

## MATUMIZI YA AI KATIKA USIMULIAJI UPYA WA MIGHANI YA TOM MBOYA

*Fred Simiyu (Chuo Kikuu cha Kibabii)*
*Noah Majele (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Ingawa akiliunde imetumika sana katika sekta nyingine kama afya, mawasiliano, elimu na siasa, kuna matumizi machache katika taaluma ya fasihi simulizi. kuna ugiligili kuhusu namna ambavyo akiliunde inaweza kuzalisha picha, video na sauti za majagina ambao wamesahaulika kutokana na mpwito wa wakati. kumbe, akiliunde inaweza kutumiwa katika usimuliaji upya wa ngano, haswa zile za majagina. Makala hii inanuia kuonesha namna ambavyo akiliunde inaweza kutumiwa kusimulia upya ngano ya Tom Mboya, mmoja kati ya magaina maarufu katika nchi ya Kenya. Uchambuzi wa data utaongozwa na Nadharia ya Wingi-Mifumo kwa lengo la kuhuisha masimulizi ya Tom Mboya kwa kutumia zama mahsusi za akiliunde

## NAFASI YA AKILI UNDE KATIKA UTAFITI NA UCHAPISHAJI WA KISWAHILI

*Sangai Mohochi (Chuo Kikuu cha Kibabii)*
*Noah Majele (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Kasi ya maendeleo ya kiteknolojia inayoshuhudiwa ulimwenguni imeathiri nyanja mbalimbali za maisha. Utafiti na uchapishaji, ambayo huchangia pakubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha, yamekuwa kigezo muhimu katika kupima ufanisi wa lugha katika utekelezaji wa majukumu yake. Akili Unde imeibuka kuwa na mchango mkubwa katika harakati za utafiti na uchapishaji katika lugha mbalimbali. Katika Kiswahili, utafiti na uchapishaji, kama ilivyo kwa lugha zingine ulimwenguni, umejikuta katika mazingira hayo ya matumizi yanayoongezeka ya Akili Unde. Hata hivyo, hakuna tafiti nyingi ambazo zimefuatilia nafasi hiyo ya Akili Unde kwa kina. Makala hii imelenga kutalii nafasi ya Akili Unde katika utafiti na uchapishaji wa Kiswahili, ikiwa ni pamoja na changamoto zinazobainika katika matumizi hayo. Utafiti huu utaongozwa na Nadharia ya Uamuzi wa Kiteknolojia. Data za utafiti zitakusanywa kupitia usaili utatumika kukusanyia data, ambapo watumiaji wa Akili Unde watakaoteuliwa maksudi kutokana na matumizi yao ya Akili Unde watasailiwa. Data zitachanganuliwa na kuwasilishwa kwa maelezo. Uchunguzi huu unatarajiwa kubainisha hali ya matumizi ya Akili Unde katika utafiti na uchapishaji wa Kiswahili pamoja na changamoto zinazowakumba watumiaji wake. Fauka ya hayo, unatarajiwa kuonesha mikakati inayotumiwa katika kukabiliana na changamoto hizo.

## UCHUNGUZI WA KONGOO ZA VYOMBO VYA HABARI VYA KISWAHILI KWA KUTUMIA AI NA ISIMU YA KONGOO: MKABALA WA ISIMU-HABARI

*Hezekiel Gikambi Peter (Chuo Kikuu Cha Kenyatta)*

Katika enzi ya kidijitali, vyombo vya habari vya Kiswahili vinashiriki nafasi kuu katika ujenzi wa diskosi za umma, hasa kuhusu masuala ya kijamii, kisiasa, na kitamaduni. Hata hivyo, utafiti wa kina unaotumia mbinu za Akili-Unde (AI) na Uchakataji wa Lugha Asilia (NLP) kuchambua maandiko haya kwa wigo mpana umekuwa adimu. Utafiti huu unapendekeza njia bunifu inayounganisha AI na Isimu ya Kongoo kwa mtazamo wa Isimu-Habari ili kufichua mikakati ya lugha, mitindo ya mawasiliano, na mitazamo ya ki-ideolojia katika vyombo vya habari vya Kiswahili—kuanzia magazeti na televisheni hadi mitandao ya kijamii. Kwa kuunda sampuli ya kongoo thabiti ya maandiko haya na kutumia zana za AI, utafiti utachambua kikompyuta vipengele vya sarufi, msamiati, na maudhui, kuangazia jinsi vinavyowakilisha mada kama utawala, utambulisho, na mabadiliko ya kijamii. Pia utatathmini jinsi vyombo hivi vinavyoathiri maoni ya umma na ujenzi wa utambulisho wa kitaifa.

.

Kwa Hisani ya
Chama Cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani
(CHAUKIDU)

## CHAI

## SAA 4:30 – 5:00 ASB



## MAHALI: AUD C (UKUMBI MKUU)

## MWENYEKITI: KIARIE WA'NJOGU

# FURSA ZA AKILI UNDE KATIKA TAALUMA YA KISWAHILI: MFANO WA VYUO VIKUU

**JUMANNE**
**5:00 ASB – 5:50 ASB**



**Isaac Ipara Odeo**
*Makamu Mkuu wa Chuo*
*Chuo Kikuu cha Kibabii*

Prof. Isaac Ipara Odeo ni Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kibabii. Anajulikana kwa mchango wake mkubwa katika uongozi wa taasisi za elimu ya juu, maendeleo ya tafiti, na kukuza ubora wa ufundishaji katika vyuo vikuu. Akiwa na taaluma pana katika elimu na utawala wa vyuo, Profesa Ipara ameongoza taasisi kadhaa kwa umahiri, na ameheshimika kwa kuimarisha mifumo ya kitaaluma, kuendeleza miundombinu ya vyuo na utafiti, na kusukuma mbele ajenda za ubunifu katika elimu ya Afrika Mashariki. Prof. Odeo ni msomi na mwanazuoni na mdau mkubwa sana wa Lugha ya Kiswahili. Katika makala haya maalumu, Profesa Odeo atazungumzia fursa na "vizingiti mbalimbali vinavyojitokeza kwa uzito mkubwa katika elimu ya Kiswahili."

**Mada: AI, Kamusi, na Istilahi**
**Mwenyekiti: Jonathan Choti**
**Mahali: ABB 015**

## NAFASI YA AI KATIKA UUNDAJI ISTILAHI NA KAMUSI THANIYA YA KISWAHILI - KICHINA: FURSA NA CHANGAMOTO

*Mussa M. Hans (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)*

Kwa muda mrefu sasa kamusi za Kiswahili ikiwa ni pamoja na kamusi thaniya zimekuwa zikitungwa kwa kuzingatia mbinu jadia. Hata hivyo, mbinu hizi zimekuwa zikiboreshwa kila uchao. Mathalani, kuna wakati utunzi wa kamusi ulifanyika kwa kuanza kuandika vidahizo katika kadi na baadaye matumizi ya kompyuta yalipoimarika matumzi ya kadi yakaachwa. Kazi ya uandishi, usanifu na uhifadhi wa kamusi ikaanza kufanywa kwa kutumia Komputa. Hivi sasa matumizi ya teknolojia ibuzi ikiwamo AI yanazidi kuimarika kila uchao. Kwa kawaida kamusi thaniya mbali na mambo mengine zinaandikwa ili kukidhi mahitaji ya jamii kutokana na mwingiliano wa jamii hizo. Miongoni mwa jamii ambazo zimekuwa na mwingiliano wa karibu ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na wazungumzaji wa lugha ya Kichina. Kuimarika kwa mwingiliano huo kunaukilia haja ya kuimarishwa kwa njia ya mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa jamii hizo. Hivyo makala haya yanalenga kuangazia namna ambavyo AI inaweza kusaidia katika kuimarisha uhusiano wa jamii ya Waswahili na Wachina kupitia utunzi wa kamusi thaniya ya Kiswahili na Kichina. Makala yataangazia fursa zilizopo, changamoto na namna ya kukabiliana nazo. Makala haya yatakuwa ni sehemu ya mradi mpana wa kuimarisha uhusiano wa jamii hizi kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ibuzi ikiwamo AI.

## UIMARISHAJI WA KAMUSI ZA KISWAHILI KUPITIA AKILIUNDE: NAFASI NA CHANGAMOTO

*Sarah Ndanu Ngesu (Chuo Kikuu cha South Eastern)*

Licha ya ongezeko la matumizi ya Kiswahili Kitaifa na Kimataifa, maendeleo yake katika kamusi za kidijitali zinazotegemea Akiliunde (AI) yamesalia kuwa katika kiwango cha chini. Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi Akiliunde inavyosaidia katika uundaji wa kamusi za Kiswahili. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Isimu Kongoo, utafiti ulitathmini uwezo wa Akilimnemba katika kuandaa kamusi kiotomatiki, kusasisha maana, na kuboresha usahihi wa matumizi ya maneno. Data zilikusanywa kupitia mahojiano na wataalamu, uchambuzi wa kamusi za dijitali za Kiswahili zilizopo, na hojaji kwa watungaji na watumiaji. Washiriki waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Data za kimaelezo zilichambuliwa kimada, huku maoni ya watumiaji yakichambuliwa kitakwimu. Matokeo yanaonesha kwamba kuna uhitaji wa matumizi ya zana zinazotumia Akiliunde. Aidha, utafiti umeonesha kwamba kuna changamoto za uhaba wa kongoo za Kiswahili. Inapendekezwa kuwekeza katika kukuza kongoo za Kiswahili, API huria, na ushirikiano wa watunga kamusi na wazungumzaji asilia wa Kiswahili.

## AI, TAFSIRI NA UKALIMANI KATIKA MAWASILIANO YA LUGHA

*Richard Makhakha Iyaya (Chuo cha Kiislamu Uganda)*

Mawasiliano ni mchakato wa kupashana au kubadilishana mawazo, maoni, hisia au habari kwa maneno, maandishi au ishara ili kufikia lengo au mwelekeo uliokusudiwa na kukubaliwa. Huweza kutoa na kubainisha maana na muktadha mawasiliano. Tafsiri hulenga kujaza pengo kati ya lugha tofauti, kupitisha maana na muktadha na kukuza uelewano wa kiulimwengu kupitia lugha hizo. AI hulenga kuimarisha, kuendeleza, kuboresha uthabiti na ukamilifu, na kuwezesha miundo mipya ya mawasiliano ya binadamu. Fafanuzi hizi zinazua ari ya kiutafiti kulenga kubainisha mwingiliano wa majukumu ya tafsiri/ ukalimani na AI pamoja na kuainisha athari yake katika kurahisisha uelewa katika mawasiliano. Nadharia ya Tafsiri ya Mashine ya *Neural* (NMT) iliyojikita katika kujifunza kwa kina na mitandao ya neva bandia. Malengo yatakuwa kubainisha majukumu ya tafsiri na AI; kuainisha mwingiliano wa tafsiri na AI, na kujadili athari ya mwingiliano wa tafsiri na AI katika mawasiliano hasa ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Kwa kujumuisha tafsiri na AI, wataalamu wa lugha, utafiti na mawasiliano wataweza kuzindua njia na vifaa muhimu vya mawasiliano ambavyo vitaweza kuvunja vizuizi katika lugha, kukuza maelewano, na kuendeleza mwingiliano wa kilimwengu.

**Mada: Kiswahili, AI, na Siasa**
**Mwenyekiti: Hezekiel Gikambi**
**Mahali: ABB 016**

## MATUMIZI YA KISWAHILI NA AKILI UNDE KATIKA UANAHARAKATI KATIKA MITANDAO YA KIJAMII

*Juliet Jagero (Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia)*

Katika zama za kidijitali, mitandao ya kijamii imekuwa jukwaa muhimu la uanaharakati kwa kuwezesha uhamasishaji wa haraka na ushiriki wa kitaifa na kimataifa. Makala hii inachunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili na Akili Unde (AI) katika uanaharakati katika majukwaa ya mitandao ya kijamii. Lugha hutumika kama nyenzo muhimu ambayo wanaharakati huwasilisha ujumbe wao, kuleta mshikamano, na kueleza changamoto zinazoibuka. AI, kwa upande mwingine, ina jukumu la ama kuwezesha au kutatiza uanaharakati. Nchini Kenya, uanaharakati katika mitandao ya kijamii umezidi kuendelezwa kupitia matumizi ya AI kupinga, kutaarifu na kutahadharisha umma kuhusu masuala ibuka. Utafiti huu unachunguza jinsi AI imesaidia katika kufanikisha au kukwaza uanaharakati kupitia uundaji upya na ubadilishaji wa video, sauti na picha. Picha, video na sauti zitakazochunguzwa ni zile ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili na kuzingatia masuala yanayofanyika nchini Kenya. Data zitakusanywa kutoka mtandao wa X na facebook. Kipindi kitakachohusishwa ni mwaka wa 2024 hadi 2025. Data zitachanganuliwa na kuelezwa ili kudhihirisha namna uanaharakati unafanywa kupitia IA huku lugha ya Kiswahili ikitumika kama nyenzo muhimu.

## KISWAHILI NA LUGHA ASILIA ZA KIAFRIKA: AKILI UNDE, CHANGAMOTO YA KISIASA NA MWELEKEO WA DIJITALI.

*Jaika Patrick (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Lugha ni kitambulisho cha kitaifa na kisiasa. Katika Afrika ya Mashariki, Kiswahili kimezidi kuwa lugha rasmi, lakini lugha asilia zinaonekana kupotea katika sera na mawasiliano kidijitali. Hatua za hivi karibuni za kudijitalisha lugha za Kiafrika, hususan Kiswahili, zimekabiliwa na changamoto za kisiasa, uvumbuzi wa akili unde na ukandamizaji wa lugha asilia kupitia sera zinazoegemea Kiswahili na Kiingereza pekee. Hali hii imezifanya lugha za kiasili zilizo na wasemaji wachache kuhatarika na hata kutoweka. Hata hivyo ni muhimu kuchambua hali ya Kiswahili na lugha hizo za kiasili katika siasa na teknolojia. Zana za Akili Unde zinaweza kusaidia kuandika, kutafsiri, na kuhuisha lugha za asili, lakini mara nyingi zinapendelea lugha zilizo na data nyingi. Utafiti huu unalenga kuchambua mitazamo ya kisiasa, kiteknolojia na matumizi ya lugha hizi za kiasili ukizingatia changamoto za upungufu wa rasilimali na ushindani wa lugha ya kigeni kwenye majukwaa ya digitali. Utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani. Wahusika 100 kutoka lugha za asilia za Kiswahili, Kinandi na Lutiriki walihusishwa. Nadharia ya haki za kiisimujamii ya Robert Phillipson na wenzake (1999-2000) ilitumiwa. Matokeo yanaonyesha kuwa sera za kujumuisha lugha nyingi, ujenzi wa kopora, na programu maalum za mafunzo ni muhimu kuunga mkono lugha za Kiafrika.

## VITA VYA MEME: MEME ZA MTANDAONI KAMA UPINZANI NA UIMARISHAJI WA ITIKADI INAYOTAWALA

*Gladys Kinara (Chuo Kikuu cha Kibabii)*

Meme za mtandao zimeibuka kama mojawapo ya majukwaa muhimu ya sanaa ya kisasa. Mbali na kusambaa kwa haraka, zimeunganisha ucheshi na kejeli kwa lengo la kuathiri namna wanajamii wanavyowasiliana na kutangamana na masuala ya kijamii mtandaoni. Kando na jukumu lao la kuburudisha, meme zimepanuka na kuwa zana za usemi wa kiitikadi zinazosheheni maudhui ya kisiasa, kijamii na kitamaduni. Kwa kutumia nadharia ya hejimonia ya Antonio Gramsci, nadharia ya Louis Althusser inayoangazia vyombo vya dola na ile ya Michel Foucault inayoangazia usemi, makala hii itachunguza namna meme ama zinaunda, kuendeleza au kupinga miundo ya mamlaka na utambulisho wa wanajamii katika mazingira ya kidijitali. Makala hii itatumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo ili kubainisha usambazaji, usawiri wa mamlaka na mienendo ya nguvu za mamlaka katika majukwaa ya mtandaoni. Usampulishaji utafanywa kimaksudi ili kupata data itakayofanikisha makala hii. Matokeo yanatarajiwa kuonyesha kuwa meme ni nyenzo muhimu zinazoweza kubomoa simulizi kuu kwa kuibua ukinzani lakini pia zinaweza kutwaliwa na majukwaa yanayoendeshwa na dola au nguvu za kikapitalisti hivyo kuimarisha itikadi tawala.

**Mada: Kiswahili, AI, na Siasa**
**Mwenyekiti: Benitha France**
**Mahali: ABB 0114**

## UAMILIFU WA AKILI MNEMBA KATIKA USANIFISHAJI NA UPANUZI WA ISTILAHI ZA KISWAHILI KATIKA NYANJA MAALUM

*Riro Matinde Samwel (Chuo Kikuu cha Kisii)*

Makala hii inalenga kuchunguza namna akili mnemba (AI) inavyoweza kuendeleza usanifishaji na upanuzi wa istilahi za Kiswahili katika nyanja maalum za utaalamu kama vile; teknolojia, tiba, sheria, uhandisi, TEHAMA, kilimo cha kisasa, elimu miongoni mwa nyingine. Ukuzaji wa istilahi sahihi ni muhimu kwa kuwezesha matumizi sahihi ya Kiswahili katika nyanja za kisasa na kuongeza uelewa wa kitaalamu miongoni mwa watumiaji wa lugha. Sababu kuu ya kufanya utafiti huu ilitokana na mwitikio mdogo wa Kiswahili katika mazingira ya kitaalamu yanayoendelea kidijitali. Kwa kutumia nadharia ya uundaji istilahi za kisayansi na nadharia ya semantiki kitaalamu, utafiti uliangazia nafasi ya akili mnemba katika kuchambua, kubuni, na kusanifisha istilahi. Data kwa ajili ya makala haya ziliksanywa kwa kutumia mbinu mseto: uchambuzi wa kimaudhui, ushirikishwaji wa mifumo ya akili mnemba kama vile *ChatGPT,* na ukusanyaji wa maoni ya wataalamu wa lugha. Makala hii inaonyesha kuwa AI inaweza kuongeza kasi na ubora wa usanifishaji wa istilahi, kutoa istilahi mpya zinazozingatia muktadha na dhima mahsusi, na kukuza utumiaji wa Kiswahili kama lugha ya kitaalamu. Matokeo ya utafiti huu ni mchango wa pekee kwa tafsiri za kitaalamu, usawazishaji wa istilahi, na sera za lugha katika enzi ya kidijitali.

## KISWAHILI, AI, UHURU WA TEKNOLOJIA NA UMAJUMUI WA MWAFRIKA

*Gordien Ndayikengurukiye (Chuo Kikuu cha Ualimu cha Burundi)*

Bara la afrika linahitaji mambo mengi ili lijikomboe kifikra na kufikia mendeleo endelevu. Moja ya mambo hayo ni kuwa na lugha moja ya kuunganisha waafrika ili kushirikiana kama wana wa Afrika. Huo ni umajumui na uliokuwepo tangu miaka ya 1945 na ambao ulifikisha afrika kupata uhuru. Tunaweza kujivunia kuwa kipo Kiswahili kinachotambuliwa kama lugha ya mwafrika mweusi miongoni mwa watu wengine duniani. Japo kuwa kipo, ipo pia Akili Unde ambayo inatawala dunia nzima na matumizi yake ni huru katika zama za teknolojia lakini pia inatumiwa na watu aghalabu wengi hasa afrika. Ipo kwenye simujanja ama andoroidi, ambazo zipo mikononi mwa mtu kila wakati. Akili Unde ina uwezo unaofananishwa na akili ya binadamu na uwezo huo unaendelea kuwezeshwa zaidi. Teknolojia hiyo ina wenyewe na haipo huru kutumiwa bila sharti. Kuna fursa nyingi za kuitumia ili kuendeleza lugha na utamaduni wa waafrika lakini uhuru wa kuitumia ukoje? inasaidia? inasaidia kujenga au kupotosha maarifa? zipo changamoto zinazohitaji kujadiliwa. Mkala hii inalenga kuonyesha fursa za kuitumika na changamoto zake. Data zitapatikana kwa usomajimatini mtandaoni na hojaji. data hizo zitachambuliwa kwa kutumia Nadharia ya kutimiza ya mwanaisimu na mhakiki wa fasihi Wolfang Iser ya mwaka 1979 na kufasiri matokeo ya mahojiano.

## NAMNA AI INAVYOATHIRI UWASILISHAJI WA FASIHI YA KISWAHILI

*Charles Kiarie Mburu (Chuo Kikuu cha Egerton )*

Makala haya yanachunguza kwa kina namna ambavyo teknolojia ya akili bandia (AI) inabadilisha, kuunda, na kusambaza fasihi ya Kiswahili. Uchunguzi unaongozwa na nadharia ya Baada ya Ubinadamu (post-humanism). Nadharia hii inalenga kuvunja mipaka ya kimawazo inayomtenganisha binadamu na mashine, na kuangalia uhusiano wa ushirikiano kati ya viumbe wa kibinadamu na mfumo wa kiteknolojia. Katika enzi ya kidijitali, AI inajitokeza si tu kama nyenzo ya kiufundi bali pia kama mshiriki hai katika michakato ya ubunifu wa kazi za kifasihi. Makala hii imegawanywa katika sehemu kuu zinazoshughulikia muktadha wa kihistoria wa fasihi ya Kiswahili na teknolojia, misingi ya nadharia ya baada ya ubinadamu, mifano ya miradi ya AI inayohusiana na Kiswahili, changamoto zinazojitokeza, na fursa zinazoweza kutumiwa ili kukuza fasihi ya Kiswahili katika zama hizi za maendeleo ya kasi ya teknolojia.

**Mada: Kiswahili, AI, na Siasa**
**Mwenyekiti: Leonora Anyango**
**Mahali: ABB 0115**

## NAFASI YA AKILI UNDE KATIKA MCHAKATO WA TAFSIRI (KISWAHILI - KIINGEREZA)

*Musa Elias Mashaka (Chuo Kikuu cha Dodoma)*

Makala inajadili namna akili mnemba inavyojitokeza kama nyenzo muhimu ya muktadha wa kisasa katika mchakato wa tafsiri ya maandiko kutoka lugha moja kwenda nyingine. Utafiti uliozaa makala hii ni wa kimaktaba. Mbinu ya uchambuzi wa matini imetumika katika ukusanyaji wa data, ambapo maandiko yanayohusu matumizi ya akili mnemba katika lugha, tafsiri na teknolojia yalitathminiwa kwa kina. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui, huku Nadharia ya Ufunuaji Maana iliyoasisiwa na Friedrich Schleiermacher (1768–1834), ikitumika kama mwongozo wa mjadala huu. Makala inabainisha kuwa akili mnemba inajitokeza kama chombo chenye mchango katika kuharakisha mchakato wa tafsiri, kupunguza gharama na kuongeza upatikanaji wa tafsiri kwa urahisi zaidi. Aidha, changamoto kama ukosefu wa uelewa wa muktadha, kiutamaduni, matumizi yasiyo sahihi ya msamiati wa Kiswahili na ukosefu wa ubunifu wa kifasihi huathiri kwa kiwango kikubwa ubora wa tafsiri inayozalishwa na akili mnemba. Kwa kuzingatia mjadala huu, inapendekezwa kuwa tafiti zaidi zifanywe kwa kutumia tafsiri halisi za maandiko ya Kiswahili na kuchunguza jinsi akili mnemba inavyoweza kuunganishwa na kanuni za Kiswahili. Kupitia tafiti hizo, itajengeka misingi ya kuunda akili mnemba yenye uwezo wa kutafsiri kwa kuzingatia utamaduni na muktadha wa msamiati wa lugha ya Kiswahili.

## AI DARASANI: NAFASI, MATARAJIO NA UHALISIA WA MATUMIZI YA AI KWA LUGHA YA KUFUNDISHIA

*Moses Wamalwa Wasike (Chuo Kikuu cha Alupe)*
*Benson Sululu (Chuo Kikuu cha Kibabii )*

Utafiti huu unachunguza mitazamo ya walimu kuhusu matumizi ya akili mnemba (AI) na viwango vya matumizi yake katika mazingira ya ufundishaji darasani, hasa kwa kuzingatia lugha ya kufundishia. Katika enzi hizi za mageuzi ya kiteknolojia, AI inazidi kupewa nafasi kama nyenzo ya kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Utafiti ulitumia mbinu mseto ili kuchambua maoni ya walimu, maandalizi yao, na hali halisi ya matumizi ya zana za AI katika ufundishaji kwa kutumia lugha rasmi za kufundishia. Matokeo yalionesha mitazamo tofauti—kutoka kwa waliokuwa na matumaini makubwa hadi kwa waliokuwa na shaka au hofu—ambapo tofauti hizi zilitegemea mambo kama vile ujuzi wa kiteknolojia, msaada wa taasisi, na uelewa wa faida za AI katika muktadha wa lugha ya kufundishia. Ingawa baadhi ya walimu wameanza kutumia AI kusaidia ujifunzaji wa kibinafsi, tathmini ya kiotomatiki, na majukumu ya kiutawala, wengine bado hutumia kwa kiwango cha chini kutokana na ukosefu wa mafunzo au kutoelewa jinsi AI inaweza kuimarisha matumizi ya lugha darasani. Utafiti unasisitiza haja ya mafunzo mahsusi kwa walimu na sera thabiti zitakazowawezesha kutumia AI ipasavyo katika kufanikisha malengo ya elimu kupitia lugha ya kufundishia. Matokeo haya yanatoa mwongozo kwa programu za mafunzo ya walimu, maendeleo ya mitaala, na tafiti za baadaye.

## AKILI UNDE, TEKNOLOJIA, NA UKUZAJI WA KISWAHILI

*Richard Makhakha (Chuo Kikuu cha Laikipia )*

Lengo kuu la kazi hii ni kuainisha uhusiano na umuhimu wa Akili Unde, tekinolojia na ukuzaji wa Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika katika zama za AI. Karatasi itashughulikia malengo yafuatayo: kubainisha uhusiano uliopo kati ya Akili Unde na teknolojia; kuainisha namna Akili Unde na tekinolojia inavyokuza Lugha ya Kiswahili, na kujadili nafasi na changamoto katika utafiti wa Akili Unde, tekinolojia na ukuzaji wa Kiswahili. Huu utakuwa utafiti wa maktabani. Ukuzaji wa karatasi hii utaongozwa kwa Nadharia ya Utata inayohusu ukuzaji lugha kwa mfumo wa Akili Unde na teknolojia. Kulingana na Uhl-Bien na Marion na wengine (2009), Nadharia ya Utata husababisha vipengele dhahiri kutokana na kuwa na mwingiliano mkubwa, isiyo na maana inayofanana na isiyoonekana kutabirika. Matokeoya karatasi hii yatawafaidi wasomi, watafiti, wakuza sera na waandishi wa isimu na lugha wataweza kubainisha maadili ya Akili Unde na kuendeleza uingilugha mtandaoni, kuhamasisha sauti za Waafrika katika kukuza na kusababisha maingiliano yenye maana katika mfumo wa akili Unde kijamii, kieneo na kilimwengu.

# JUKWAA LA LUGHA ZETU: TAFITI NA MATUMIZI YA AI

## KATIKA MBINU SHIRIKISHI ZA UHIFADHI NA UENDELEZAJI WA LUGHA NA LAHAJA ZA KIAFRIKA

AI imeibuka kama nyenzo ya kimapinduzi iwezayo kutumika katika kuhifadhi, kuendeleza, na kufundisha/kujifunza lugha. Kwa hakika, mapinduzi haya yanapaswa kulifaidisha bara la Afrika ambamo, japo zaidi ya theluthi moja ya lugha na tamaduni zote duniani imo humo, lugha nyingi miongoni mwa hizo zinapotea na kukosa umuhimu kwa sababu ya ushindani utokao kwa lugha za kikoloni na lugha nyengine kubwa za kikanda. Wasilisho hili litaangazia jinsi ambavyo mapinduzi ya kiteknolojia yaletwayo na AI yanaweza kutumika kama wenzo muhimu wa kuzihifadhi na kuziendeleza lugha za Kiafrika. Hoja kuu zitahusu jinsi uwekezaji katika Modeli Kubwa za Lugha (MOKULU) yaani Large Language Models (LLMs), Uchakataji wa Lugha Asilia (ULUA) yaani Natural Language Processing (NLP), Tafsiri za Mashine yaani Machine Translation, na matumizi ya zana za kutambua na kubadili usemi na maandishi yaani speech-to-text/text-to-speech tools viwezavyo kuwa nyenzo muhimu katika mkakati huo. Washiriki watajadili jitihada na mkakati wa Jukwaa lao (Jukwaa la Lugha Zetu) katika kuzihifadhi, kuziendeleza, kuzifundisha au kujifunza lugha na lahaja zinazotoweka barani Afrika. Wasilisho hili linasisitiza kuwa AI si tishio bali ni fursa ya kuandika upya historia ya lugha na utamaduni wa Kiafrika kwa vizazi vijavyo. Lengo ni kuhamasisha ushiriki wa wataalamu na jamii katika kutumia AI kama chombo cha kuzifufua, kuzikuza, na kuzihifadhi Lugha Zetu na tamaduni zao.

## MAHALI: UKUMBI WA WARSHA

## MWENYEKITI: ALWIYA OMAR



**Alwiya Omar**
*Chuo Kikuu cha Indiana, Marekani*

## WANAJOPO

*Abdilatif Abdalla (Msemaji/Mwandishi wa Kimvita)*
*Filipo Gao Lubua (Chuo Kikuu cha Pittsburgh)*
*Hadija Jilala (Chuo Kikuu Huria cha Tanzania)*
*Leonard Muaka (Chuo Kikuu cha Howard)*
*Mwanahija Juma (Baraza la Kiswahili la Zanzibar)*
*Zainab Iddi (Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar)*

# CALLiT Africa
## We Bring Your Global Learning Vision to Life

**Our programs are:**

- Flexible and responsive to your needs
- Academically aligned
- Culturally immersive

**CALLiT AFRICA**
Computer-Aided Lasting Learning

Find us in Tanzania and Kenya.
We've Partners all over Africa.



At CALLiT Africa,we design customized study abroad programs that match the goals of both students and instructors. Whether you're seeking culture - rich academic immersion, outdoor experiential learning, or faculty-led travel courses, we make it happen.

*Partner with us to co-create a transformative African learning journey tailored just for your group*

CALL NOW
+255 762 448 403
director@callitafrica.com
www.callitafrica.com
PANDA ADVENTURES

# USIKU WA MSWAHILI
# NA
# TUZO ZA UENEZI

**MAHALI: Hoteli ya Siri Tamu**

**12:30 Jioni – 5:59 Usiku**

*Andaa Tumbo lako*
*na*
*Viatu vya Dansi ☺*

A

*Abdilatif Abdalla, 37*
*Aidah Mutenyo, 13*
*Alwiya Omar, 37*
*Andrew Watuha, 23*
*Anna Mwalagho, 24*
*Anyonje Florence, 27*

B

*Beltha Ntanwa, 14*
*Benard Okal, 14*
*Benitha France, 13, 35*
*Benson Sululu, 36*
*Bernard Oginga, 21*
*Betty Nasambu, 28*

C

*Caroline Asiimwe, 19*
*Charles Mburu, 35*
*Cleophas Sikolia, 15, 22*
*Consolata Mushi 19*

D

*David Wanyonyi, 23*

F

*Fabiola Hassan, 21*
*Filipo Gao Lubua, 5, 10, 19, 37*
*Flora Malema, 27*
*Fred Simiyu, 8, 13, 28, 30*

G

*Gladys Kinara, 28, 34*
*Gordien Ndayikengurukiye, 30, 35*

H

*Hadija Jilala, 37*
*Hamisi Babusa, 29*
*Happy Buzaaba, 18*
*Hezekiel Gikambi, 30, 34*

I

*Iribe Mwangi, 3, 7*
*Isaac Ipara Odeo, 17*

J

*Jaika Patrick, 34*
*Jonathan Choti, 33*
*Juliet Jagero, 34*
*Justus Makhokha, 23*

K

*Kiarie Wa'njogu, 32*
*Keneth Inyani Simala 17, 32*

L

*Leonard Muaka, 37*
*Leonora Anyango, 29, 36*
*Lorna Mwijarubi, 22*

M

*Mahiri Mwita, 18*
*Mary Ndung'u, 13*
*Michael Wairungu, 21, 28*
*Mokaya Bosire, 22*
*Moses Wasike, 15, 22, 36*
*Mosol Kandagor, 21, 23, 28*
*Muhtari Athmani, 14, 29*
*Musa Mashaka, 36*
*Mussa Hans, 3, 6, 15, 33*
*Mwanahija Juma, 28, 37*
*Mwanaisha Omar, 15*

N

*Noah Majele, 30*
*Nyabuto Choti, 16*

O

*Olivia Kanwa, 27*

P

*Patrick Mose, 18, 19*
*Patrick Oyinda, 22*
*Peter Mwangi, 3, 4*
*Priscah Kiprotich, 27*

R

*Rayya Timammy, 16, 23*
*Richard Makhakha, 33, 36*
*Riro Matinde Samwel, 35*
*Rose Mavisi, 24*

S

*Saade Said Mbarouk, 28*
*Sabushimike Ezéchias, 14*
*Sangai Mohochi, 30*
*Sarah Ngesu, 16, 23, 33*
*Sarah Vincent, 29*

V

*Vinold Mkenda, 16, 24, 28*

Z

*Zainab Iddi, 37*
*Zelda Sam, 15*